SportPesa
TZS. 686,934,380
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**KESI YA MBOWE**

**Uamuzi** wa kupokea, kutopokea kielelezo kutolewa J'tatu

UKURASA 3



**Spurs hawana mpango na Bale**

UKURASA 22

Nipashe
Ijumaa Novemba 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580769
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# TANESCO yafunguka kukatika kwa umeme

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**UJUMBE WANAOSITA CHANJO YA CORONA**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewashauri watu ambao bado wanasita kupata chanjo ya corona, kubadili...

UKURASA WA 5

**TANZANIA NA KENYA ZAAFIKIANA HUDUMA MAGONJWA YA DAMU**

WATAALAMU wa afya wa Kenya na Tanzania wamekubaliana huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ya...

UKURASA WA 5

**SERIKALI YAWATOA HOFU MAGOMENI KOTA**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, amewatoa hofu wakazi wa Magomeni Kota wanaotarajiwa...

## Nyumba mganga zahanati yachomwa, mjamzito akifariki

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua pazia kuzindua rasmi mnara wa kumbukumbu ya jubilei ya maadhimisho ya miaka 50 ya Hospitali ya Bugando jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, akipokea zawadi maalum kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (watatu kulia), baada ya kuzindua huduma ya Benki ya CRDB inayozingatia misingi ya kiislamu 'CRDB Al Barakah', jijini Zanzibar jana. Wengine ni Waziri wa Fedha Zanzibar, Jamali Kassim (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Ally Laay (wapili kulia) na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bernard Kibesse. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Samia awa mbogo uhaba maji

• **Awatangazia** vita wanaoharibu vyanzo, makali mgawo yazidi kung'ata Dar...

*Endelea ukurasa 2&4*

**MICHEZO** **SIMBA, RUVU TAMBO ZATAWALA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Chapa wa Mamlaka ya Bandari ya Singapore, Eugene Tay, kuhusu namna wanavyotumia teknolojia katika kurahisisha upakiaji na upakuaji makasha, alipotembelea katika bandari hiyo, jana. **PICHA: OWM**

# TANESCO yaanika sababu kukatika umeme

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limetoa sababu kuhusu kukatika kwa umeme huku ikibainisha kuwa ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyofanya kupungua kwa maji, hivyo kushuka kwa uzalishaji wa nishati hiyo katika mabwawa yake.

Taarifa hiyo ya TANESCO imetolewa ikiwa imepita miezi miwili tangu Waziri wa Nishati, January Makamba, alipofanya ziara ya kushtukiza makao makuu ya shirika hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi huku kukatika mara kwa mara kwa umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika ziara hiyo, Makamba aliagiza shirika hilo ndani ya wiki mbili kuhakikisha linamaliza tatizo hilo.

TANESCO kupitia taarifa yake jana, ilisema uzalishaji wa umeme kwenye mabwawa umepungua kwa megawati 345 sawa na asilimia 21, kutokana na kupungua maji kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Uhusiano Makao Makuu, upungufu huo umeathiri uzalishaji wa umeme katika vituo vyake vya Kihansi, Kidatu na Pangani.

Kutokana na hali hiyo taarifa hiyo ilisema: "Shirika linachukua hatua za haraka kuongeza uzalishaji kwa kutumia gesi asilia, kwa kuharakisha matengenezo ya baadhi ya mitambo yake ya Ubungo I wenye megawati 25, upanuzi wa Kinyerezi 1 megawati 185 na Ubungo III Megawati 112.

"Hatua hiyo itaenda sambamba na kuwashwa kwa kituo cha Nyakato chenye megawati 36 na kwamba suala hilo litasaidia kuongeza jumla ya megawati 358."

"Kwa kuwa kutakuwa na upungufu kwa baadhi ya mikoa taarifa zitatolewa kwa wakati ili wateja waweze kupanga kazi zao. Tunawaomba radhi wateja wetu kwa usumbufu unaojitokeza," iliongeza taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizoko uzalishaji wa umeme kwa sasa nchini ni megawati 1,605 zinazotokana na megawati 900 gesi, maji megawati 508 na nishati jadidifu megawati 58.

**MAAGIZO YA WAZIRI**

Septemba 17, mwaka huu, Makamba alitembelea makao makuu ya TANESCO na kutoa wiki mbili kuhakikisha hakuna tatizo la kukatika umeme nchini.

Licha ya kutoa agizo hilo, Makamba alionya kuwa atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake na malalamiko ya kukatika kwa umeme yakiendelea kujitokeza, wahusika wote watachukuliwa hatua.

"Ndani ya wiki mbili sitaki kusikia kukatika kwa umeme nikisikia kuna malalamiko nitachukua hatua kwa wahusika walioshindwa kutekeleza wajibu wao," alisema Makamba.

# Ujumbe wanaosita chanjo ya corona

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewashauri watu ambao bado wanasita kupata chanjo ya corona, kubadili msimamo wao ili kuiwezesha serikali kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19.

Alitoa rai hiyo jana katika hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji jijini Arusha, iliyosomwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, aliyemwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amechukua hatua kadhaa kuhakikisha ugonjwa huo hauendelei kuwa kikwazo kwa maendeleo ya uchumi wa nchini.

Katika hotuba yake hiyo, Dk. Mpango alisema hatua muhimu kwa sasa ni utoaji wa chanjo ya corona kwa wananchi. "Hii ndiyo njia sahihi iliyothibitika ya kukabiliana na baa hili wakati jitihada zingine zikiendelea. Ningependa kuwahimiza wale ambao bado wanasita kuchanja, kufanya uamuzi sahihi wa kukubali kupata chanjo ya UVIKO-19.

"Chanjo zinapunguza madhara ya UVIKO-19 kwa asilimia 90 kama mtu ataambukizwa ugonjwa huu.

"Idadi ya watu nchini inakadiriwa kuwa milioni 59, tumefungua uchumi wetu kwa soko la Afrika Mashiriki lenye idadi ya watu milioni 200.

"Uchumi wetu unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.8 mwaka 2022 kutokana na mikakati ya uwazi na uwajibikaji inayotekelezwa na serikali pamoja na kuimarika kwa sekta ya utalii na kufunguliwa kwa mipaka baada ya athari za janga la UVIKO-19," alisema.

Aliongeza kuwa Rais Samia ameshaweka bayana kwamba atahakikisha uwazi na uwajibikaji unakuwapo kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma kwa kuweka wazi takwimu na ripoti zinazohusu rasilimali za nchi. Alisema Rais Samia pia anaendelea kuwawajibisha watendaji wa serikali wanaobainika kufuja mali ya umma.


MOPEH COMPANY LIMITED

,+255 0785 335544 , 0713 639979, 0673 335528, P. O. Box 32372 Dar es Salaam – TANZANIA
Mob. +255 (0)785335544, +255(0)673335528, +255(0)755731072, Email: info@mopeh.co.tz, mopehltd20@gmail.com Web: www.mopeh.co.tz

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED** tunatoa muda wa siku 14 kwa mdaiwa aliyeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini awe amelipa deni analodaiwa na benki pamoja na gharama za Kampuni, kunyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali iliyowekwa kama dhamana ya mkopo aliokopa kwa mujibu wa mkataba husika. Mnada utafanyika sehemu mali ilipo, siku na tarehe kama itakavyotangazwa kwenye vipeperushi na gari la matangazo.

| TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 04/12/2021 | 10;30 ASUBUHI | KISWIGU MPYANGA BERNALD/SHOKII IBRAHIMPISHOKI T/A SK TWINS PARK HOTEL | HOTELI ILIYOPO,HATI MILIKI NAMBA 160894 MG, KIWANJA NAMBA 36,KITALU B, BAGAMOYO MJINI ILIYO NA JINA LA KISWIGU MPYANGA BERNARD | BAGAMOYO MJINI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa malipo ya asilimia 25% ya fedha taslim papo hapo baada ya nyundo ya dalali, na ndani ya siku 14 toka siku mnada mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 75% ya salio.
2. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo na sehemu ilipo.
3. Mnunuzi atakaposhindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
4. Mali / dhamana zitauzwa kama zilivyo.
5. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba zilizohapo juu au nenda tawi lolote la **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED** lililo karibu nawe.


# Samia awa mbogo uhaba wa maji

**Na Richard Makore,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amegeuka mbogo kuhusu uhaba wa maji nchini huku akiwatangazia vita wanaohujumu vyanzo vya maji na kusababisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kukumbwa na adha ya huduma hiyo.

Kutokana na tatizo hilo, Rais Samia amewaagiza wakuu wa mikoa kuanza kuwasaka wote wanaofanya hujuma hiyo. Rais Samia aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya jubelei ya miaka 50 ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa ya Bugando yaliyofanyika jijini hapo huku akitaja mambo manne yanyochangia kuwapo uhaba wa maji katika maeneo mbalimbali hususan Dar es Salaam na Pwani.

Alitaja mambo hayo ni watu kunywesha ng'ombe katika vyanzo vya maji huku akibainisha kuwa ng'ombe mmoja ana uwezo wa kunywa lita 40 za maji, hivyo ikitokea mfugaji akawa na kundi kubwa na mifugo, kuna uwezekano akapunguza maji.

Sababu nyingine, kwa mujibu wa Samia, ni watu kuchepusha maji kwenye mito kwa ajili ya kilimo. Alisema katika mito mbalimbali, watu wamefunga mashine kubwa za kuvuta maji kwa ajili ya umwagiliaji, hivyo kusababisha wengine kukosa au kupata kidogo. Jambo la tatu, alisema ni ukataji wa miti katika sehemu mbalimbali za nchi kwa ajili ya ufugaji na kwamba wafugaji wanafanya hivyo ili kuona mifugo yao kwa zaidi ya kilomita sita inapokuwa inachungwa. Sababu ya nne, kwa mujibu wa Rais, ni mabadiliko ya tabia nchi kutokana na mambo mbalimbali ambayo mengine yanatokana na shughuli za kibidamu.

**ASHTUKA ONGEZEKO SARATANI**

Kuhusu saratani, Rais Samia alishtushwa na ongezeko kubwa la wgonjwa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuagiza ufanyike utafiti wa kina ili kubaini chanzo chake.

Kwa mujibu wa takwimu, asilimia 60 ya wagonjwa wanaofika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam, wanatoka Kanda ya Ziwa.

Alisema kuna sababu nyingi zinazotajwa kusababisha ugonjwa wa saratani, ikiwamo matumizi ya zebaki inayotumika kwenye migodi, lakini akahoji kwa nini shida hiyo ni kubwa kwa wanawake. Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Hospitali ya Bugando, Renatus Nkwande, alisema wanakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi 1,300.

Pia alisema wanahitaji jengo la wagonjwa wa nje ambalo linatarajiwa kugharimu Sh. bilioni tano ili kukidhi mahitaji kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa.Aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwaondolea kodi mbalimbali ili kuwahudumia wananchi vizuri. Rais Samia aliahidi kulifanyia kazi ili kuona namna bora ya kulipatia ufumbuzi wake.

Naye Rais wa Baraza la Maskofu Tanzania (TEC) na Askofu Mkuu wa Kanisa katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga, alisema Rais Samia ameonyesha moyo wa kuwatumikia wananchi.

Askofu Mkuu Nyaisonga alisema hospitali hiyo kwa sasa inaendeshwa kwa ubia kati ya serikali na Kanisa Katoliki kwa makubaliano maalum.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Bugando, Dk. Fabian Massaga, alisema hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 1971 na kwamba wazo la kuanzishwa lilikuwa la Hayati Mwalimu Julius Nyerere ili kupambana na adui maradhi kwa Watanzania.

HABARI KITAIFA

## KESI YA MBOWE

# Uamuzi wa kupokea, kutopokea kielelezo kutolewa Jumatatu

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Jumatatu wiki ijayo inatarajia kutoa uamuzi mdogo kwenye kesi ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (pichani) na wenzake watatu wa kupokea kielelezo cha kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam (DR) au kukataa.

Hatua hiyo ya Mahakama imekuwa ikitokea mara kwa mara kwenye shauri hilo kutokana na kuibuka kwa malumbano ya kisheria wakati kesi ikiendelea.

Mahakama mbele ya Jaji Joackim Tiganga, ilimaliza kusikiliza hoja za pande zote mbili na upande wa utetezi ulikuwa ukipinga kielelezo hicho kilichotakiwa kutolewa na shahidi wa pili kwenye kesi ndogo, Askari H4323 Koplo Msemwa, kupokelewa kwa madai utaratibu haukufatwa.

Wakili Jeremiah Mtobesya alidai ahitaji kuzunguka sana kuhusu hoja hiyo, alidai kitu kikishaingia mahakamani utaratibu wa kukitoa ni uleule uliotumika kama kilivyoingia na kwamba amri ya mahakama inahitajika.

"Nilimsikia kaka yangu Wakili Abdallah Chavula akidai shahidi wa kwanza alipokuwa anaomba kielelezo Mahakama iliwaruhusu apewe, bila kuingilia kilichofanyiwa basi ni ukiukwaji mkubwa wa taratibu za Mahakama.

"Kama kweli Mwenendo wa shauri uko sawasawa kwanini wanaomba mahakama ipokee tena DR kwa mara ya pili, kitendo cha kuomba ipokelewe tena na Mahakama ni ushahidi tosha kwamba hili shauri tofauti.

"Sababu za kupinga pingamizi letu zinakosa mashiko, tunaomba mahakama isizingatie kabisa hoja za Jamhuri zisizo na mashiko," alidai Mtobesya.

Akiongeza hoja Wakili Peter Kibatala, alidai upande wa Jamhuri walikuwa na nafasi tangu mara ya kwanza kama walitaka kukitumia kielelezo hicho walipaswa kuomba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Pius Hillar, akiongezea majibu kwa upande wa Jamhuri alidai mtitiriko umeelezwa vizuri kwenye ushahidi, msingi wa namna kielelezo DR kimemfikiaje shahidi umeelezwa vizuri.

Alidai kwa kutambua mazingira yote hayo kuhusu pingamizi za upande wa utetezi hakuna hoja nzito ya kuzuia kielelezo hicho kupokelewa kuingia mahakamani.




"Tunaomba mapingamizi yatupiliwe mbali, kielelezo kipokelewe na tuendelee na usikilizwaji wa shauri," alidai Hillar.

Baada ya kumaliza kuwasilisha hoja, Jaji Tiganga aliomba dakika kumi za kutathmini hoja ili kujua uamuzi atatoa lini.

Mahakama iliporejea, Jaji Tiganga aliahirisha kesi hadi Jumatatu kwa ajili ya kutoa uamuzi wa kupokea DR ama la.

Hatua iliyopo katika shauri hilo ni usikilizwaji wa kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi iliyoibuka baada ya mawakili wa utetezi kupinga kupokelewa kwa maelezo ya onyo ya mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya.

Upande wa utetezi ulitoa hoja kwamba mshtakiwa aliteswa na kusainishwa maelezo katika Kituo cha Polisi Mbweni na kwamba hajawahi kufikishwa Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam Agosti 7, mwaka 2020 kama inavyodaiwa na upande wa Jamhuri.

Ili kuondoa sintofahamu hiyo Mahakama iliamuru kuingia katika kesi ndogo, upande wa Jamhuri una mashahidi sita na Koplo Msemwa ni shahidi wa pili.

Katika kesi hiyo washtakiwa ni Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanakabiliwa na Mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

# Nyumba ya mganga wa zahanati yachomwa moto

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Nkundi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wameichoma moto nyumba ya mganga wa zahanati ya kijiji hicho kwa kilichodaiwa ni hasira kutokana na mganga huyo kutokaa kituoni.

Imeelezwa kuwa hasira hizo zilichangiwa na mjamzito kupoteza maisha kituoni hapo bila mganga huyo kuwapo.

Akizungumzia tukio Dilo Diwani wa Kata ya Kipande, Joseph Mwenda, alisema kuwa tukio hilo lilitokea hivi karibuni ambapo wanakijiji walichoma moto nyumba ya serikali ambayo alikuwa akiishi mganga huyo, Marco Lazaro.

Diwani huyo alisema kuwa kwa muda mrefu wanakijiji wamekuwa wakimtuhumu mganga huyo kuwa hakai kituoni, kitendo kinachowasababishia kukosa huduma kwa wakati na kulazimika kusafiri kwenda maeneo mengine kutafuta huduma.

Diwani Mwenda alisema kutokana na malalamiko hayo, waliwahi kupeleka malalamiko kwa mwajiri wake, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa, hivyo kuwakasirisha wanakijiji hao wananchi hao wakisema kwa muda mwingi hakuwa kituoni kutoa huduma.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Nkansi, Benjamin Chota, alisema kuwa baada ya tukio hilo yeye na wataalamu wengine wa afya walifika kijijini hapo na kushuhudia nyumba hiyo ikiwa imechomwa moto na baadhi ya wanakijiji.

Alisema alichoamua ni kumwondoa mganga huyo na kumrudisha makao makuu ya wilaya na kumwagiza awe anaripoti ofisini kwake kila siku wakati ikisubiriwa taarifa ya kamati iliyoundwa kuchunguza tukio na tuhuma hizo, na kwamba taarifa hizo zitakabidhiwa kwa mwajiri wake kwa ajili ya hatua zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, William Mwakalambile, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa halmashauri hiyo imekuwa ikisikiliza malalamiko ya wananchi na kuchukua hatua.

Alisema kwa kiendo cha mganga wa zahanati huyo kutokuwapo eneo lake la kazi bila taarifa ni utoro na hakitafumbiwa macho, na kwamba kosa hilo lipo ndani ya mamlaka ya halmashauri, hivyo muda si mrefu utatolewa uamuzi.


**DIRECT MAINTENANCE TANZANIA LIMITED**

**The companies Act, 2002 (Section 334)**

**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **DIRECT MAINTENANCE TANZANIA LIMITED** a company with registration number **93129** dully convened a meeting on 7th June, 2021 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1) (b) of the Companies Act, 2002 that the company be wound up voluntarily.

All parties concerned and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **ALAIS RUNDYA MWASHA of Basil & Alred, Ace Building, Haile Selassie Road, P.O. Box 78661, Dar es salaam, Tanzania,** who is appointed Liquidator of the Company.

**Any claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.**

**ALAIS RUNDYA MWASHA**
**Liquidator**
**For DIRECT MAINTENANCE TANZANIA LIMITED**

116576801



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE COMPANIES ACT, 2002**
**COMPANY LIMITED BY SHARES**

**SPECIAL RESOLUTION OF THE MEMBERS OF DIRECT MAINTENANCE TANZANIA LIMITED**
**REG:93129**

Whereas the shareholders of Direct Maintenance Tanzania Limited (hereinafter referred to as **"The Company"** with registration number 93129 are desirous of voluntarily winding up the Company.

**IT WAS RESOLVED.**

1. That the Company be voluntarily liquidated and dissolved as decided by members.
2. That Alais Rundya Mwasha be and is hereby appointed as a liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company.
3. That Basil & Aired be and is hereby appointed auditor for the purpose of auditing the Liquidator's account of the winding up of the affairs of the Company.

**MARIA WILHELMINA BRASSE**
**CHAIRMAN**
Date: 7th June, 2021

**JOHN CHARLES REIDY**
**COMPANY SECRETARY**
Date: 7th June, 2021

116576801




Mkurugenzi Mkuu mpya wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose (kulia), akizungumza na mtangulizi wake, Hisham Hendi, jijini Dar es Salaam, ambapo alielezea vipaumbele vyake, ikiwamo kuhakikisha uendelevu wa biashara kwa kuzingatia faida, mahusiano na wadau pamoja utunzaji wa mazingira na tabia endelevu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makali ya mgawo wa maji yazidi kung'ata D'salaam

**Na Waandishi Wetu**

MAKALI ya mgawo wa maji jijini Dar es Salaam, yameshika kasi huku baadhi ya maeneo wananchi wakikosa huduma hiyo kwa zaidi ya wiki moja na bei ya galoni la lita 20 imefika Sh. 1,500.

Aidha, katika baadhi ya maeneo, hakuna maji kwa takribani siku tano hali inayowalazimu wengi kutumia maji ya visima ambayo nayo yamepanda bei kufikia Sh. 500.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Maji, Juma Aweso, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kugawa maji kwa usawa.

Hivi karibuni, ratiba ya mgawo wa maji iliyotolewa na DAWASA kwa maeneo tofauti ilionyesha kuwa maji yatatoka kwa wiki siku za Jumanne, Alhamisi, Jumamosi na Jumapili kwa muda wa saa 10 kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 1:00 jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mosi Joshua, mkazi wa Tabata Bima, alibainisha kuwa katika eneo hilo maji hutoka mara mbili kwa wiki na kwa saa chache kinyume cha ratiba ya DAWASA.

Joshua alisema hali hiyo imesababisha uhitaji wa maji kuwa mkubwa huku bei zikizidi kupaa kutoka Sh. 200 hadi 1,000 na maeneo mengine Sh. 1,500 kwa dumu lenye ujazo wa lita 20.

"Upatikanaji wa maji umekuwa ni changamoto kubwa katika eneo hili kila mtu analalamika maji. Kwenye ratiba ya mgawo walionyesha siku yakitoka yanakaa saa 10, lakini imekuwa tofauti kwani siku zingine yanatoka ndani ya saa moja yanakatika.

"Hiyo inasababisha uhaba wa maji kuzidi kuwa mkubwa kwani hata yakitoka yanakuwa machache ukilinganisha na mahitaji. Unaishia kuchota ndoo mbili, hizo zitumike kupikia, kuoga, kufulia watoto na matumizi mengine, kwa uhalisia wa kawaida ni jambo gumu," alisema.

Maeneo mengine ni Mwenge kutokana na uhaba wa maji, bei ya galoni imeongezeka kutoka Sh. 300 hadi 1,000 kwa maji ya chumvi na Mbezi kutoka Sh. 250 hadi 500. Baadhi ya maeneo ya Salasala upatikanaji wa maji umekuwa mgumu kiasi cha baadhi ya maeneo kumaliza wiki moja bila huduma hiyo.

Pia baadhi ya maeneo yanatoka usiku wa manane ambao ni hatari kwa mtu kutoka kuteka maji huku wengine wakinunua kwa kati ya Sh.500 hadi 1,000 na wengine wanauza maji ya DAWASA.

Elihudi Shabani, mkazi wa Mbezi Juu, alisema kwa mujibu wa ratiba ya DAWASA maji yalipaswa yatoke mara moja kwa wiki kila Jumanne na alidai kuwa ni zaidi ya mwezi sasa hayajatoka.

"Kutokana na uhaba wa maji ya bomba watu wengi wamekuwa wakitumia maji ya boza/chumvi ambayo awali yalikuwa yanauzwa Sh. 12,000 kwa tangi lenye ujazo wa lita 1,000 lakini gharama imepanda hadi Sh. 20,000 kutokana na uhitaji kuzidi kuwa mkubwa," alisema Shabani.

**WAZIRI AFUNGUKA**

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso akizungumza na uongozi wa DAWASA kuhusu mgawo wa maji, alisema mamlaka hiyo ihakikishe mfumo wa ugawaji unarejea kawaida.

"Niwasisitize watumishi wa mamlaka kufanya kazi usiku na mchana na kuhakikisha mgawo wa maji unatolewa kwa uwiano bila upendeleo," aliagiza Aweso.

Aliongeza kwa kuitaka DAWASA kutoa bei elekezi kwa watoa huduma binafsi wa maji kupitia magari (bowser), ili kuondoa sitofahamu iliyojitokeza kwa baadhi ya watu kuanza kuuza maji kwa bei zao wenyewe kwa kukiuka utaratibu uliowekwa na mamlaka husika.

Pia, Waziri Aweso aliahidi ushirikiano baina ya wizara na DAWASA katika kukabiliana na changamoto zilizopo kwa kuhakikisha watu wote wanapata maji kwa wakati na mgawo kuwa na uwino sawa kila sehemu.

**MBEYA WALALAMIKA**

Jijini Mbeya baadhi ya maeneo wanalazimika kutumia maji ya visima kutokana na kukosekana kwa maji ya bomba na sasa wananunua kwa Sh. 500 ndoo ya lita 20.

Mkazi wa Manenane, Clinton Swilla, alisema upatikanaji wa maji ni changamoto kubwa hali inayowafanya kutokuwa na uhakika na bidhaa hiyo.

Naye Mkazi wa Lwambi, Angelica Sulusi, alisema ni wiki ya pili sasa hakuna maji na kuiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mbeya kushughulikia kwa haraka tatizo na kuweka wazi kama kuna mgawo au la.

Katika taarifa yake kwa umma, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Neema Stanton, alisema sababu ya kukosekana kwa maji mara kwa mara ni kutokana na kukatika kwa umeme.

**Imeandikwa na Maulid Mmbaga (DAR), Grace Mwakalinga, MBEYA**

## Washauri mabadiliko mfumo wa elimu

**Na Romana Mallya**

WADAU wa watoto na vijana wameiomba serikali kufanya mabadiliko katika mfumo wa elimu kwa kupitia upya mitaala na mifumo ya shule ili kurahisisha utoaji wa elimu bora.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dar es Salaam katika mkutano baina ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), waandishi wa habari na wadau wengine wanaotetea makundi hayo kwenye jamii.

Mkutano huo uliwakutanisha pia makundi rika, ulikuwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 75 ya UNICEF.

Mwakilishi kutoka Agenda ya Watoto na Vijana, Nabiha Kassim Ali, alisema serikali na wadau wanahitajika kuchukua hatua za haraka za kuhakikisha makundi hayo yanapata elimu bora itakayowawezesha kufikia malengo yao ya baadaye.

Alisema sekta ya elimu inakabiliwa na matatizo ambayo yanasababisha watoto kutofanya vizuri kwa wingi katika mitihani yao ya kitaifa na wakati mwingine kuwa na wahitimu wasio na uwezo.

Derrick Mwakyeja ambaye ni mmoja wa vijana machampioni waliofika katika mkutano huo, alisema serikali na wadau wanapaswa kuongeza nguvu katika upatikanaji wa elimu ya huduma za afya ya uzazi ili kuwawezesha watoto na vijana kujitambua na kujikinga dhidi ya madhara na magonjwa.

Alisema kutoa elimu ya afya ya uzazi na jinsia na stadi za maisha kwa vijana waliopo shuleni na katika jamii kutasaidia kupunguza tatizo la mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia.

Mwakyeja alibainisha kuwa vijana wengi wanajihusisha na tabia hatarishi za kujamiiana, zinazowaweka katika hatari ya kupata mimba za utotoni na magonjwa ya zinaa ikiwamo VVU/UKIMWI, na kwamba kundi hilo likipata taarifa na huduma sahihi za afya ya uzazi litajiepusha na matatizo hayo.

Championi mwingine wa vijana, Said Aman, aliitaka serikali kuja na mikakati zaidi itakayosaidia kuzalisha fursa nyingi za ajira kwa vijana. Awali, wakati wa hotuba yake ya ufunguzi, Mkuu wa Huduma za Maji Kujisafisha na Kunawa Mikono (WASH) kutoka UNICEF, Tanzania, Francis Odhiambo, alieleza dhamira ya shirika hilo kuendelea kukuza haki za watoto ambazo ni pamoja na kutetea malezi bora na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji TEF, Salim Salim, alisema wanahabari wataendelea kutetea haki za watoto na vijana kupitia uchapishaji wa makala za elimu na vipindi vya runinga ambavyo vitasaidia kuelimisha jamii. Alisema kuwa TEF inaitaka serikali kulichukulia kwa uzito suala la mitaala ya shule na kufanya mageuzi makubwa yatakayosaidia kuchagiza utoaji wa elimu bora nchini.

Mjumbe mwingine wa TEF, Jesse Kwayu, alisema kunahitajika mjadala wa kitaifa kujadili kwa kina namna ya kurekebisha mfumo wa elimu.

Ofisa Mkuu wa Maendeleo ya Jamii katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Christabella Ngowi, alitaja programu ambayo inasimamiwa na idara yao kuwa ni ya Taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto ambayo itazinduliwa mwishoni mwa mwaka huu inayolenga kumkuza ili afikie utimilifu wake.

## HABARI KITAIFA



Mfanyabiashara mdogo maarufu machinga, akihamisha meza yake ya biashara eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. Kwa sasa wamachinga wanaendelea kuondoa meza na vibanda vyao kwa hiari yao katika maeneo yasiyoruhusiwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DC Gondwe awatoa hofu Magomeni Kota

**Na Halfani Chusi**



MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (pichani), amewatoa hofu wakazi wa Magomeni Kota wanaotarajiwa kukabidhiwa nyumba zao hivi karibuni kuwa hakuna mtu tofauti na wao atakayeingia katika nyumba hizo.

Gondwe aliyasema hayo jana mkoani Das es Salaam alipokuwa akizungumza na mamia ya wakazi waliokuwa wamekusanyika maeneo ya kota hizo kwa ajili ya kuendelea kupokea semina elekezi ya namna ya kuishi kwenye makazi hayo mapya.

Alisema ameamua kuyasema hayo kutokana na wimbi la matapeli wanaozuka mitaani na fomu za bandia kwamba wanaweza kupangisha watu upya.

"Nyumba hizi ni kwa ajili ya wakazi 644 na si vinginevyo. Serikali iko makini, hakuna mtu tofauti na ninyi atakayeingia katika nyumba hizi. Tunataka tuwahakikishie mnayoyasikia mitaani yale siyo, sikieni kutoka katika meza hii hapa. Tunaangalia wale waliondoka miaka mitano iliyopita ili kurudi katika nyumba zao.

"Nayasema haya ili watu waamini kwamba anachokifanya mtendaji mkuu ndicho ambacho mkuu wa wilaya anakifahamu. Hao wenye fomu za bandia huko mitaani washindwe na walegee mara moja," alisema.

Katika hatua nyingine, Gondwe aliwataka wakazi hao kuzingatia usafi na utunzaji wa mazingira pindi watakapohamia katika nyumba hizo.

"Eti kuna watu wanasema baada ya mwaka mmoja tu mazingira yatakuwa machafu yameharibika nikamwambia wewe umeanza unafiki. Wenyewe wakazi wa Magomeni wanajua nini maana ya usafi kwa hiyo niwaombe muwe wasafi na mtunze mazingira msiniangushe. Katika hilo inapofikia muda wa usafi fuateni utaratibu wa usafi," alisisitiza.

Mtendaji Mkuu Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daudi Kondoro, alitaja mchanganuo wa wakazi wanaotakiwa kurejea katika nyumba hizo.

"Wakazi 150 walikuwa watumishi na walikuwa wakiishi hapo kabla ya kubomolewa, hivyo nao hawa wametambuliwa na watarudi. Lakin kuna wakazi 336 hao ni warithi wa wakazi halali waliokuwa wakiishi hapo kabla ya umauti kuwafikia nao wametambuliwa.

"Pia wakazi 98 walikuwa wana mikataba ya kuishi kwenye nyumba hizo kabla hazijabomolewa nao wametambuliwa na watarejeshwa na kuna nyumba tisa zilikuwa zimepangishwa Ofisi ya Rais walikuwapo mpaka pale ofisi zilipobomolewa. Ziko pia nyumba 44 mmiliki wake ni zaidi ya mmoja hivyo kwenye eneo hilo panahitaji ushirikiano wa kutosha kwa wanakota ili kufanya utambuzi sahihi zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa Nyumba za Magomeni Kota, George Abeli, alimshukuru mkuu wa wilaya kufika eneo hilo na kumhakikishia hawatokuwa tayari kumvumilia mwanakota yeyote atakayekuwa mharibifu katika miundombinu ya nyumba hizo.

# Tanzania, Kenya zakubaliana huduma magonjwa ya damu

**Na Romana Mallya**

WATAALAMU wa afya wa Kenya na Tanzania wamekubaliana huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ya damu (himofilia na selimundu) zitolewe kwa kiwango kikubwa kwenye hospitali za umma ili walengwa wazipate wakati wote wanapozihitaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Damu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Stella Rwezaula, alisema hilo ni moja ya makubaliano yaliyotokana na kikao cha wataalamu hao kilichokaa kwa siku tatu kuanzia Novemba 15, mwaka huu kujadili magonjwa hayo.

Kikao hicho kimefanyika baina ya Wizara ya Afya ya Kenya na Tanzania, Kamati ya Usimamizi wa Mradi ya Hospitali ya Muhimbili na Chama cha Himofilia cha Kenya na Chama cha Wagonjwa wenye Himofilia Tanzania.

Dk. Rwezaula ambaye ni msimamizi wa mradi wa kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma kwa watu wenye magonjwa hayo, alisema kupitia mradi huo wamekubaliana wagonjwa hao ni jukumu la serikali hivyo huduma inapaswa kuongozwa na kutolewa na wizara za nchi hizo.

"Japo msaada kutoka kwa wafadhili ni muhimu katika kuanzisha au kuboresha huduma na tiba kwa wagonjwa, lakini ufadhili wa kudumu kutoka serikali husika ni muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu," alisema.

Pia alisema wamekubaliana ni lazima kuanzishwa kwa sera ambazo zitakuwa chachu ya kuboresha utambuzi na uchunguzi wa himofilia na selimundu.

"Mpango mkakati wa serikali ni muhimu ili kuongeza uelewa na utendaji kwa watunga sera, vyama vya wagonjwa vina hazina ya wataalamu wenye uwezo hivyo watumike kusaidia Wizara za Afya za Kenya na Tanzania kama washirika katika uhamasishaji na kuongeza uelewa wa ugonjwa," alisema.

Kadhalika alisema wamekubaliana kanzi data ni muhimu katika kufanya uamuzi, hivyo nchi hizo ziboreshe ubora na wingi wa taarifa za magonjwa hayo kupitia miongozo iliyopo.

Kuhusu gharama za matibabu alisema wamekubaliana jumuiya za kimataifa kushirikishwa kwa ajili ya msaada zaidi ili kupunguza mzigo.

Dk. Rwezaula alisema nchi hizo zimekubali kubadilishana uwezo baina ya wataalamu waliopo kupitia kamati ya ushauri wa matibabu iliyoundwa.

Mratibu wa chama cha mradi wa kupambana na magonjwa hayo kutoka Kenya ambaye ni mtaalamu wa magonjwa hayo katika Hospitali ya Kenyatta, Dk. Kibet Shikuku, alisema endapo wataalamu watapiga kelele kuhusu gharama kubwa za matibabu itasaidia ili zishushwe.

Mwakilishi wa selimundu kutoka Kenya, Eunice Owino, aliitaka jamii itambue kuwa magonjwa hayo wameyapata kwa kurithi kutoka kwa wazazi na kuwataka wasiwatoroke na kuwaacha wenyewe.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chanjo ya UVIKO 19 muhimu kwa afya zetu

**TANZANIA** imeingia kwenye orodha ya nchi zilizokubali chanjo ya ugonjwa wa corona, na sasa watu wake wanachanja baada ya kuhamasishwa na kuamini kuwa chanjo ni muhimu kwa afya zao.

Hatua ya kuchanja sasa inaonyesha dhahiri kuanza kuondoa dhana potofu iliyokuwapo awali kabla ya uhamasishaji na elimu ya umma, ambayo ilichangiwa na upotoshaji uliokuwa unafanywa na baadhi ya watu.

Kwa sasa viongozi wanaongoza kwa mfano wa kuvaa barakoa kila wanapokuwa kwenye mikusanyiko, na sasa imekuwa siyo jambo la ajabu kwa mtu kuvaa mbele za watu.

Viongozi wameonyesha kwa mfano kwa kuchanja hadharani kiasi cha dozi ya awali kufika nchini ya Jonson and Jonhson kutokana Marekani kumalizika kabla ya Desemba 2, mwaka huu, ambayo ilielezwa ingeharibika. Pia, zimekuja chanjo za aina nyingine mbili za Sinopharm kutoka China, ambazo zinaendelea kusambazwa kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini.

Tayari wataalamu wa afya wameeleza faida za chanjo kuwa ni kuongeza nguvu ya kinga ya mwili ili kuuwezesha mwili kupambana na maradhi hasa ya UVIKO-19, na siyo kwamba huwezi kupata bali utakuwa katika nafasi ya kupona zaidi kuliko ambaye hajachanja.

Kwa aliyechanja akipelekwa hospitali kwa ajili ya corona ana nafasi kubwa ya kupona au kutozidiwa kwa kuwa askari wa zaidi waliotangulia mwilini wataongeza mashambulizi kwa adui aliyeingia mwili na mwisho kuwa salama.

Yapo maneno mengi kuhusu corona, ambayo siyo kweli kwa kuwa wataalamu wa afya na wanasayansi kwa ujumla wameshathibitisha kuwa chanjo za COVID-19 zilizopitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), hazina madhara kwa binadamu kwa kuwa zimefanyiwa utafiti wa kutosha.

Aidha, maudhi madogo madogo yanaweza kujitokeza baada ya kutumia ambayo huwa ya muda mfupi sana na baadaye yanatoweka, huku wengi wakishauriwa kumweleza mtoa huduma hali ya afya yake kabla ya kupata chanjo.

Kuna umuhimu mkubwa kwa kila kiongozi kuanzia mkuu wa mkoa na wilaya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tarafa, katibu kata na watendaji wa vijiji na mitaa kutoa elimu sahihi kwa umma.


Pia, ni wajibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuendeleza jitihada za kutoa elimu kupitia vipeperushi, mabango na ujumbe mbalimbali ambao utawafikia wananchi moja kwa moja na kufanya uamuzi.

Tunaona jitihada za kutumia vyombo vya habar, lakini bado wananchi wanataka kuona viongozi wakiwafuata na hata kuonyesha mfano wa kuchanjwa kwa kuwa wapo ambao hawajachanjwa. Ikiwa tutafanikiwa kuchanja wengi au Watanzania wote, kasi ya maambukizi au kuugua na kuzidiwa itapungua na kuokoa Watanzania wengi zaidi.

Hakuna ubishi kuwa ukichanjwa huwezi kupata UVIKO-19 na ndiyo maana wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari ikiwamo kuvaa barakoa, kuepuka misongamano, kunawa mikono kwa vitakasa mikono au maji na sabuni muda wote. Kila mmoja akiwajibika atahakikisha wa karibu yake naye anapata chanjo na kuondoa dhana potofu dhidi ya chanjo ambayo imekuwapo miongoni mwa watu.

Kwa maisha ya sasa chanjo haiepukiki na tangu watoto hadi utuuzima tumechanjwa chanjo nyingi ambazo hakuna aliyehoji, lakini hii kumekuwa na habari nyingi za kupotosha na huu ndio wakati umuhimu wa kuwapa wananchi taarifa sahihi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hii nenda rudi ya machinga, ni kutaka kutii sheria kwa shuruti

Na Sabato Kasika

**WAFANYABIASHARA** wadogo, maarufu 'machinga' wameondolea katika maeneo mbalimbali yasiyo rasmi jijini Dar es Salaam, ambako waliyatumia kufanya shughuli zao.

Machinga hao waliondolewa mwishoni mwa mwezi uliopita na kuelekezwa kwenda kwenye masoko yao ambayo wametengewa na manispaa mbalimbali zilizomo mkoani Dar es Salaam.

Ingawa wamehamishwa, kwa kuondoa vibanda vyao, baadhi wanaendelea kuwapo kwenye maeneo hayo wakipanga bidhaa chini kama kawaida, hali inayoonyesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika kufanikisha uhamaji wao.

Huo ni mtindo ambao wamekuja nao, huku wengine wakiwa na meza ndogo au kufunga kamba na kutunda nguo za kuuza kana kwamba kazi iliyofanywa na serikali ni kuondoa mabanda kwenye maeneo hayo, siyo wao.

Kitendo chao cha kurejea katika maeneo waliohamishwa, inawezekana ikawa ni dalili kwamba, wanahitaji kuelimishwa zaidi ili watambue kuwa biashara haipo kando ya barabara tu kama ambavyo baadhi yao wanadhani.

Ikumbukwe kuwa baadhi yao wamekuwa wakisikika wakisema hawawezi kwenda katika masoko waliotengewa, kwa madai kwamba hakuna biashara na ndiyo maana wanalazimika kupanga bidhaa zao kando ya barabara.

Ninaamini kuwa hiyo dhana si sahihi na inawezaa kudhoofisha juhudi za Rais wetu na serikali kwa ujumla, za kutaka wapangwe vizuri ili wafanye biashara zao, bila ya kubughudhi watu wengine kwa kuzagaa hadi kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Siku ya mwisho ya kuondoka katika maeneo yasiyo rasmi, ilikuwa Oktoba 18, lakini uongozi wa mkoa ukawaongezea siku nyingine 12 za kujipanga kuhama, Bado naona baadhi yao wameendelea kung'ang'ania walikoondolewa.

Kuendelea kuwapo baaadhi ya machinga kwenye maeneo walioondolewa, kunaweza kuwavunja moyo wengine ambao tayari wamehamia katika masoko, nao wakaamua kurejea walikotoka.

Hilo likitokea, linaweza kusababisha mkakati wa serikali wa kuwahamisha kuwa mgumu. Hivyo ingekuwa vyema wakatambua kuwa wateja hufuata huduma mahali na sehemu ilipo na si kandoya barabara pekee.

Wangeachana na uzoefu wa miaka ya nyuma wa kuondolewa kisha wanarudi wakati wa jioni kupanga biashara au kurejesha mabanda, huku wakiacha masoko yao ambayo wangeyaendeleza hadi yakashamiri.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba, serikali ina nia njema kutaka wafanye biashara zao katika maeneo waliotengewa wakiwa salama na kutenga bila ya kuchafua mazingira kama ambavyo imekuwa ikitokea.

Iwapo kuna jambo ambalo wanaona halijawa sawa, si vibaya wakawasiliana na uongozi wao, kuliko kila mmoja kuchukulia hatua na kurejea eneo aliloondolewa kana kwamba wana haki ya kufanya wanavyotaka.

Kimsingi, kufanya biashara kwa kufuata utaratibu ni jambo jema kuliko kulazimisha kama ambavyo baadhi ya machinga wanafanya, hali ambayo wakati mwingine inaweza kusababisha wakatii sheria kwa shuruti.

Ikumbukwe kwamba kuendelea kupanga bidhaa chini au kwenye meza, ni sawa na bado hawajaacha wazi maeneo ambayo wametakiwa kuhama, ili wapangwe vizuri katika masoko wanayoandaliwa kwenye sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Njia nzuri ingekuwa ni wao kukaa katika masoko ili wateja wazoee badala ya kwenda na kurudi kama ambavyo baadhi yao wamekuwa wakifanya na ikifika jioni huhamia kandoka ya barabara au ndani ya stendi za daladala. Yapo madai mbalimbali ambayo huwa wanayatoa ya kutaka kuboreshewa miundombinu ya masoko, ikiwamo ya maji na mingine ndipo wahamie, lakini wanahasau kuna suala la kutimiza wajibu.

Ingekuwa vyema kama wangetimiza wajibu kwa kuhama huku wakiendelea kudai kile wanachokihitaji katika masoko yao, kuliko wanachofanya sasa wanadai vitu ambavyo hata katika maeneo walioondolewa.

Katika maeneo walioondolewa, hakuna huduma ya vyoo wala maji, ndiyo maana baadhi yao hujisaidia ovyo na kuchafua mazingira.Wanapataje ujasiri wa kukataa masoko ili wabaki wakiendelea kuchafua mazingira?

Ni kweli wanahitaji kufanya biashara, lakini ingefaa iwe katika mazingira rafiki badala ya kuona eneo liko wazi na kulivamia kana kwamba hakuna taratibu, kanuni na sheria zinazoelekeza jinsi ya kufanya biashara zao.

HABARI KITAIFA

## Ununuzi vifungashio nje ulivyowaathiri wakulima

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAFANYABIASHARA wa maduka ya pembejeo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, wilayani Mbozi, mkoani Songwe, wanadaiwa kuwahujumu wakulima kwa kununua mifuko ya vifungashio nchi jirani na kuweka mbegu za kienyeji kwa madai kuwa zimefanyiwa utafiti (mbegu bora) na kuwauzia wakulima. Kufuatia tabia hiyo ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wananchi, Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Mlowo (TEO), Joel Kaminyoge, akizungumza na wenyeviti wa vitongoji katika kikao cha baraza la mamlaka hiyo, aliwaonya wafanyabiashara wanaofanya hujuma hizi.

Alisema hivi karibuni kumeibuka kundi la wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, ambao huenda kununua mifuko ya vifungashio katika nchi jirani za Zambia na Malawi kisha kuweka mbegu za kienyeji kwa madai kuwa ni mbegu bora.

"Ndugu wenyeviti pamoja na mji wetu kuendelewa kustawi vizuri, bado tumeendelea kuwa na changamoto mbalimbali za kiusalama, likiwamo hilo la baadhi ya wafanyabiashara kufanya hujuma za kuwauzia pembejeo feki wakulima na kuwasabishia hasara kubwa," alisema.

Aliwataka wenyeviti hao wa vitongoji katika mamlaka hiyo kwenda kufanya uchunguzi kwenye maeneo yao na kuwabaini wale wote wanaofanya hujuma hizo, ili mamlaka zichukue hatua za kisheria. "Tuna taarifa kuwa shughuli hizi za kufunga mbegu feki za mahindi baada ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza vifungashio toka nchi za Malawi na Zambia huwa zinafanyika katika baadhi ya misitu ya maeneo myayowaongoza na kwenye majumba wanakoishi wananchi wenu," alifafanua .

Aidha, alisema mbali na hujuma hizo, pia kuna kundi la vijana katika mji huo, ambao wameacha kufanya shughuli halali za kujipatia kipato badala yake wamejiingiza kwenye shughuli haramu za kuwa mawakala wa kusafirisha wahamiaji haramu na kuugeuza mji huo kuwa kitovu cha biashara hiyo haramu.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwatahadharisha wakazi wa Mji wa Mlowo, wilayani Mbozi ambao wanajihusisha na biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu, ikiwemo wamiliki wa nyumba za kulala wageni, ambazo zinadaiwa kutumika kuwahifadhi kabla ya kusafirishwa kwa bodaboda hadi maeneo ya mipakani.

# Mkemia mkuu atoa mwongozo kukabili kemikali zenye hatari

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imeandaa mwongozo wa namna bora ya kusimamia kemikali hatari katika maeneo ya bandari, bandari kavu, viwanda, maghala na usafirishaji wake nchini.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kikao cha wadau wanaoshughulika na usimamizi wa kemikami hatarishi kwa ajili ya kupokea maoni yatakayoboresha mwongozo huo.

Alisema lengo la mwongozo huo ni kubainisha makundi ya mizigo hatarishi, alama za utambulisho wa mizigo kulingana na tabia au sifa pamoja na kubainisha utaratibu wa kisheria unaohitajika kwa kampuni au mtu anayesimamia.

"Kampuni au mtu anayetaka kushughulikia au kusimamia kemikali hatarishi katika maeneo niliyoainisha lazima afahamu taratibu na mwongozo ambao tunauandaa kwa kupata maoni yenu," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema pia uundaji wa mwongozo huo ulizingatia nyaraka za mataifa mengine yanayosimamia na kushughulikia usafirishaji wa kemikali hatarishi.

Dk. Mafumiko alitaja baadhi ya nchi ambazo nyaraka zake zimetumika ni Canada, Thailand, Umoja wa Falme za Kiarabu na Ujerumani.

"Katika kuhakikisha tunazingatia sheria, kanuni na uzoefu wa wadau mbalimbali katika kusimamia au kushughulia mzigo hatarishi, tunaomba mtoe maoni yenu na mapendekezo ya kuboresha mwongozo huu kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa letu," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kusimamia na kudhibiti madhara yanayoweza kusababishwa na mizigo hatarishi hasa katika maeneo hatarishi.

Dk. Mafumiko alisema jitihada hizo ni pamoja na kutunga sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, sheria namba 3 ya mwaka 2003 na kanuni zake zilizofanyiwa mapitio mwaka 2020.




Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, Anthony Nyange, akifungua mkutano wa Siku ya Mtoto wa Kike kitaifa uliyoandaliwa na Taasisi ya Tanzania Coalition Against Child Labour, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SOS yakabidhi halmashauri kituo cha afya

**Na Magabilo Masambu**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Arusha imekabidhiwa kituo cha afya ambacho awali kilikuwa kikiendeshwa na shirika la SOS Tanzania.

Kituo hicho sasa kitaendeshwa na kusimamiwa na halmashauri hiyo kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya, hivyo kuwapunguzia wananchi adha ya kukosa huduma.

Akizungumza juzi wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya kituo hicho, iliyofanyika kwenye kijiji cha watoto cha SOS Ngaramtoni, Mkurugenzi Mtendaji wa SOS Tanzania, David Mulongo, alisema lengo la kuipa halmashauri ni kupanua wigo wa huduma za afya.

Mulongo alisema lengo kuu la kuanzishwa kwa shirika hilo ni kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na kuendesha miradi ya elimu na afya.

Hata hivyo, alisema kwa sasa shirika limeamua kujielekeza zaidi katika malengo yake ya awali katika kuhudumia watoto pekee na kwamba miradi ya elimu na afya itasimamiwa na wadau wengine, ikiwamo serikali.

"Naipongeza serikali kwa jitihada kubwa inazofanya katika eneo la afya kwa kuonyesha kwa vitendo kujenga zahanati kila kijiji. Nasi kama wadau wa maendeleo, tumeona tuongeze nguvu ikizingatiwa kwamba, tumekuwa na ushirikiano mzuri sana na serikali ndiyo maana tumekabidhi leo kituo hiki cha afya ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya SOS, Haruna Masebu, aliiomba serikali kuona umuhimu wa kukifanya kituo hicho cha afya kuwa cha mfano kuanzia usimamizi wake, wahudumu pamoja na huduma zitakavyokuwa zinatolewa.

"Tumekabidhi kituo hiki kwenu, tuombe basi angalau kiwe cha mfano katika halmashauri hasa kwenye utoaji wa huduma na mazingira yake," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Suleiman Msumi, aliishukuru SOS Tanzania kwa ushirikiano mzuri kwa serikali hasa katika utoaji huduma za kijamii kwa umma wa Watanzania.

Msumi alilihakikishia shirika hilo juu ya utunzaji wa kituo hicho cha afya, ikiwa ni pamoja na kuweka wahudumu wa afya wenye weledi wa hali ya juu ili kuhakikisha kinakuwa cha mfano kwa wilaya katika utoaji wa huduma zake kama ilivyoombwa na shirika lenyewe.

"Serikali inathamini sana michango ya maendeleo inayotolewa na wadau. Niwahakikishie tu kwamba kituo hiki kitakuwa cha mfano kuanzia huduma kwa wateja ambayo huwa pia ni tiba kabla ya kupata tiba yenyewe," alisema.

Hata hivyo, Msumi aliiomba SOS kuangalia uwezekano wa kupata angalau gari moja la wagonjwa kituoni hapo, lengo likiwa ni kunusuru vifo vya wagonjwa ambao watakuwa wanapewa rufani kwenda kupata matibabu kwenye hospitali za wilaya na mikoa.

# Bil.5.7/- kuanzisha kituo mafunzo upimaji na ramani

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

SHILINGI bilioni 5.75 zitatumika kuanzisha mradi wa kituo cha mafunzo katika taaluma ya upimaji na ramani zikiwa ni msaada wa serikali ya Korea Kusini.

Hayo yalibainika jana jijini hapa wakati ujumbe wa timu ya wataalamu kutoka Kampuni ya Hojung Solution Co. Ltd ya Korea Kusini uliomtembelea Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kwa lengo la kumwelezea maendeleo ya maandalizi ya uanzishwaji wa kituo hicho mkoani Dodoma.

Ujumbe huo ulioongozwa na Rais na Mtendaji Mkuu wa Hojung Solution Co. Ltd, Munseok Lee, ulimweleza Waziri Lukuvi kuwa kampuni hiyo kwa kushirikiana na kampuni nyingine ya nchini humo, Korea Land Informatix, zimeteuliwa kutekeleza mradi wa kituo hicho.

Kwa mujibu wa ujumbe huo, mradi wa kuanzishwa kituo hicho unatarajiwa kuanza Januari, mwakani na ni juhudi za serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kuhakikisha inapata wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi wa kuendesha mradi mkubwa wa kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani nchini.

Mradi huo mkubwa unaandaa ramani za uwiano mdogo na zile za uwiano mkubwa kwa miji mikuu 26 ya mikoa ya Tanzania Bara sambamba na kuweka vituo vya kielektroniki vya upiamji ardhi na kuboresha miundombinu ya kusambaza taarifa za kijografia kwa idara za serikali na watumiaji wote nchini.

Waziri Lukuvi aliueleza ujumbe huo kuwa serikali ya Tanzania kupitia wizara yake, iko tayari kushirikiana na kampuni hiyo katika kutekeleza mradi huo na hatua za haraka zitachukuliwa ili mradi uanze mapema kabla ya ule mradi mkubwa wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani nchini utakaogharimu takriban Sh. bilioni 150 kuanza.

"Niwahakikishie kuwa serikali itawapa ushirikiano wa hali ya juu katika hatua za utekelezaji mradi huu kufanyika mapema kabla ya mradi mkubwa unaotarajiwa kuanza mapema mwakani na mimi nitafuatilia kwa karibu ili nione mafanikio," alisema Lukuvi.

Mratibu wa Mradi huo, Dk. Eric Mwaikambo, alisema amefurahishwa sana na maendeleo ya maandalizi ya uanzishwaji kituo hicho kwa kuwa ndoto inakaribia kutimia.

"Nimefurahishwa sana na hatua ya utekelezaji mradi huu iliyofikiwa. Wizara chini ya Katibu Mkuu inafanya kila jitihada kuhakikisha mradi wa ujenzi wa kituo pamoja na ule mkubwa unaanza kama ilivyokusudiwa," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Erasto Kiswaga (katikati), akiongoza zoezi la uzinduzi wa huduma ya bima maalum ya kilimo ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ya kuwalinda wakulima, wavuvi na wafugaji dhidi ya hasara wanapopata majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri uzalishaji wao, wilayani humo, mkoani Shinyanga jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa wateja binafsi wa benki hiyo, Elibariki Masuke (wapili kushoto), Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Augustine Semkurutu (wapili kulia), Mwenyekiti wa SHIRECU, Kwiyolecha Mkilijiwa (kushoto) na Mwenyekiti wa WETCU, Hamza Kitunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema ya bima yaja kwa wakulima, wafugaji, wavuvi

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

WAKULIMA, wavuvi na wafugji wamepatiwa fursa ya bima, ambayo itawalinda dhidi ya hasara.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Jubilee Insurance kuzindua huduma hiyo kuyalinda makundi hayo dhidi ya hasara wanapopata majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri uzalishaji wao.

Bima hiyo ilizinduliwa jana wilayani Kahama mkoani Shinyanga na Mkuu wa Wilaya hiyo, Erasto Kiswaga, katika hafla fupi ambayo pia ilihusisha mafunzo kuhusu umuhimu na faida za bima hiyo kwa wadau mbalimbali wakiwamo wakulima na viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) kutoka mkoa huo.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa wateja binafsi Benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema ujio wa huduma hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kupitia huduma za kibenki zinazolenga kutatua changamoto zinazogusa sekta hiyo muhimu.

"Benki ya NBC tuinatambua vema sekta ya kilimo na zaidi tunatambua mchango wa wakulima katika uchangiaji wa uchumi wa nchi na kwa msingi huu tumeona ni vema kuja na bima ya mazao kwa wakulima. Bima hii ni ya kwanza nchini na tunaamini kwa dhati kwamba kupitia bima hii wakulima watapunguza kwa kiwango kikubwa hasara zitokanazo na majanga mbalimbali yasiyotabirika yaani yale yalio nje ya uwezo wao." alisema.

Alisema ujio wa huduma hiyo utawasaidia Watanzania ambao asilimia 70 wanategemea shughuli ya kilimo kwa kuwapatia uhakika wa matokeo wanayoyatarajia kupitia shughuli zao za kilimo, uvuvi na ufugaji hata pale wanapokabiliwa na majanga ya asili ikiwamo mvua ya mawe, mafuriko, ukame, upepo mkali, moto na majanga mengine ambayo yamekuwa yakiwasababishia hasara kubwa na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Kiswaga alitoa wito kwa wakulima hao kutumia fursa hiyo kukata bima ili iwasaidie kuwakinga wanapokumbwa na majanga mbalimbali, huku akiitaja sekta ya kilimo kuwa miongoni mwa sekta zinazokabiliwa na majanga mengi yasiyotabirika ikiwamo mafuriko, moto, wadudu na ukame ambavyo vimekuwa vikiwasababishia hasara kubwa wakulima.

"Hizi ni dalili njema kuona sasa huduma za bima zimeanza kuwafikia wakulima ambao kimsingi ndio kundi kubwa zaidi katika shughuli za uzalishaji hapa nchini likigusa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania. Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wa vyama vya msingi mliohuduhuria uziunduzi huu vipeleke mpango huo kwenye bodi za mazao mbalimbali ili utaratibu wa kuwalipia bima hii wakulima uanze mara moja,"

Awali akifafanua zaidi kuhusu huduma hiyo, Mkuu wa Idara ya Bima wa Benki hiyo, Benjamini Nkaka, alizitaja bima hizo kuwa ni pamoja na bima ya mazao inayohusisha mazao yote ya chakula na biashara pamoja na mazao ya matunda, bima ya mifugo inayohusisha mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi kondoo pamoja na Bima ya samaki mahususi kwa ajili ya wavuvi.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima hao Mwenyekiti wa Chama Kikuu la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema huduma hiyo imekuja wakati mwafaka katika kipindi ambacho wakulima wamejipanga kufanya mapinduzi ya kilimo kupitia kilimo cha kisasa kinachoshusisha tahadhari zote muhimu ili kuepuka hasara ambazo zimekuwa zikiwarudisha nyuma kimaendeleo.

## Watumia maji ya madimbwi

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

WAKAZI wa vijiji vitatu vya Kata ya Kakunyu Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, wanalazimika kutumia maji ya madimbwi na tingatinga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kutokana na vijiji hivyo kutokuwa na maji ya bomba.

Wakizungumzia kadhia hiyo, wakazi hao wa vijiji vya Bwenkoma, Bugango na Kakunyu walisema wanatumia maji hayo kwa muda mrefu ambayo siyo salama kwa afya zao na kuomba serikali kuwafikishia maji ya bomba.

"Lakini wakati wa msimu wa kiangazi madimbwi haya hukauka, hali hii hutufanya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 17 kufuata maji nchi jirani ya Uganda, maana vijiji vyetu vipo mpakani,"alisema Bosco Kashunju, mkazi wa kijiji Bwenkoma.

Alisema kuwa tangu uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 wamesitisha kwenda nchini Uganda kufuata maji, na kwamba sasa wanahofia zaidi usalama wa afya zao kutokana na maji ya madimbi na tingatinga wanayotumia kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

Naye, Jovitha Meshack, mkazi wa kijiji Bugango aliiomba serikali kuwasaidia kupata maji ya bomba ili kuwaondolea tatizo hilo ambalo linahatarisha afya zao, huku akidai kuwa wanaoteseka zaidi kufuata maji ni wanawake na watoto. "Ili kuwaondolea wananchi hao adha hiyo, mwaka 2014 serikali ilianza ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji hivyo uliokamilika mwaka 2018 kwa gharama ya zaidi ya Sh.milioni 875, lakini mpaka sasa mradi huo umeshindwa kutoa matumaini kwa wananchi kutokana mashine ya kusukuma maji kukosa mafuta,"alisema.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Andrew Kilembe, alikiri vijiji hivyo kuwa na adha hiyo, lakini akasema wanafanya kila jitihada kuhakikisha adha hiyo inakwisha na wananchi wanapata maji safi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

"Tunaendelea na mazungumzo na Shirika la umeme (TANESCO) ili wafunge umeme katika eneo ulipojenga mradi huo, lengo likiwa ni kuhakikisha mashine ya kusukuma maji inafanya kazi muda wote na wananchi wanapata maji ya kutosha," alisema.

## HABARI KITAIFA

## Wawekezaji waombwa kuwatumia wahitimu kutoka Chuo cha VETA

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Chuo Cha Ufundi (VETA) mkoani Pwani, Clara Kibodya, amewaomba wawekezaji wa mkoa huo kuwatumia vijana wanaofuzu mafunzo ya ufundi kutoka chuo hicho kutokana na ujuzi wanaopatiwa.

Clara alisema vijana wanaopata elimu ya ufundi katika vyuo hivyo wanakuwa wamepata elimu ya ufundi ambao wanaweza kuajirika popote na kujiajiri wenyewe.

"Mkoa wetu unaongoza kwa uwekezaji wa viwanda nchini, na sisi kila mwaka tunazalisha vijana wenye ujuzi wa fani mbalimbali ... wito wangu wawatumie kuwapatia ajira badala ya kutafuta wengine ambao wako nje ya mkoa huu," alisisitiza.

Akizungumza wakati wa mahafali ya tisa ya chuo hicho kilichopo Kongowe, alisema kwasasa wanakabiliwa na kikwazo cha kukosekana kwa magari yanayotumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kuwafundishia wanafunzi.

Alisema magari yaliyopo ni ya kizamani, hivyo kuwapa wakati mgumu wanafunzi wanaohitimu katika chuo hicho wanaporejea mitaani kutumia ujuzi waliopata.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mussa Ndomba, aliwataka vijana kujiunga na vikundi ili waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na Halmshauri hiyo.

"Ili kuondoa malalamiko ya kukosekana kwa ajira na vijana wenye fani zao kuendelea kuwa mtaani bila kazi, nawasihi wahitimu waunde vikundi vyao kulingana na fani. Mbali ya kunufaika na mikopo, pia zikitokea tenda wanapatiwa kulingana na ujuzi wao," alisema.

Mmoja wa wahitimu, Saidina Mikidadi, aliiomba Serikali kuwekeza kwenye vyuo vya ufundi ili vijana wapate ujuzi na kujiajiri badala ya kukaa kusubiri kuajiriwa.

# Marekani kuboresha elimu ya msingi Tanzania

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imeahidi kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha elimu ya msingi ili kuleta matokeo mazuri kwa watoto.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Kate Somvongsiri, wakati wa uzinduzi wa mradi wa Jifunze Ulewe, uliozinduliwa katika Shule ya Msingi ya Chifu Albart iliyopo Manispaa ya Morogoro na pia utaendeshwa kwa shule nyingine za mikoa ya Mtwara, Iringa, Ruvuma na Zanzibar.

Mkurugenzi huyo mkazi wa USAID alisema, mkakati wa Serikali ya Marekani ni kuhakikisha watoto wanajengewa msingi imara katika elimu kupitia kusoma, hesabu, kuandika na stadi za kijamii na imeamua kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Wizara ya Elimu.

Alisema ili kuunga mkono, Serikali ya Marekani kupitia USAID imelenga kuhakikisha inaboresha ubora wa elimu ya msingi kwa watoto kwa kuanza na shule katika mikoa mitano kwa kuwa ndio litakuwa taifa la kesho.

Alisema katika mpango huo pia watahakikisha walimu na wazazi wanashirikiana kwa karibu ili kuleta matokeo chanya kwa watoto ambayo yatasaidia kuboresha matokeo mazuri katika elimu.

Akizindua mradi huo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, alisema kupitia mpango huo wanafunzi wote na wenye mahitaji maalumu watawezeshwa kupatiwa vifaa vya kuwezesha kujifunzia pamoja na kutengenezewa mazingira wezeshi ya kusoma.

Waziri Profesa Ndalichako, alisema serikali imechukua hatua mahususi katika utoaji elimu kulingana na mazingira wezeshi ikiwamo kununua vitabu vya kujifunzia na kusoma pamoja na kutoa elimu kwa walimu rafiki wa watoto.

Akizungumzia kuhusu mradi huo, alishukuru Serikali ya Marekani kwa kuona umuhimu wa kusaidia kuboresha elimu katika shule ya msingi kwa kuwa itasaidi kukuza ustawi wa Watanzania katika miaka inayokuja kwa kuwa na taifa lenye vijana wenye uelewa na elimu.

Profesa Ndalichako, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi katika sekta ya elimu ikiwamo za ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajia kuanza masomo ya kidato cha kwanza mwakani.




Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando (kushoto), akimpongeza mkazi wa Mikumi, Luka Andrea Lutuli (katikati), kwa kushinda Sh. milioni 10 kutoka kwenye bahati nasibu ya Biko, katika hafla iliyofanyika katika tawi la NBC, mjini Morogoro juzi. Kulia ni Balozi wa Biko, Kajala Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA yatangaza neema ya umeme kwa wazee

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Nchini (TRA), imetangaza neema kwa wazee wenye miaka 60 wasiokuwa na uwezo wa kipato kulipwa fidia ya umeme walionunua kuanzia mwezi Julai, mwaka huu.

Kuanzia Julai mwaka huu, mteja anaponunua umeme kwa kila mwezi anakatwa Sh. 1,000 kama kodi ya majengo ambayo inakusanywa na Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) kwa niaba ya TRA.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Meneja wa TRA mkoani Mwanza, Joseph Mtandika, alisema wazee wa miaka 60 mkoani humo watarudishiwa fedha hizo kwa kipindi chote walichonunua umeme na kukatwa Sh. 1,000.

Hata hivyo, Mtandika aliliambia Nipashe kwamba wazee hao ambao kwa sasa wanaendelea kujitokeza na kujisajili ili watambulike hawatarudishiwa fedha taslimu badala yake watapewa umeme unaolingana na kiasi walichokatwa.

Alisema mpango wa mteja kukatwa kodi kila anaponunua umeme umesaidia kwa kiwango kikubwa kukusanya fedha za serikali kuanzia mwezi Julai, mwaka huu.

"Ni kweli kabisa wazee wasiokuwa na uwezo wakiwamo wastaafu hawatakiwa kulipa kodi ya majengo, kutokana na ukweli huo tutaanza kuwarudishia fedha zao kwa kuwapa umeme," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya wazee wote mkoani Mwanza kujisajili na kutambulika wataanza kurudisha fedha hizo kwa kuwapa umeme, lakini sio fedha.

Meneja huyo hakusema ni lini wazee hao wataanza kufaidika na fidia hiyo, lakini akasema usajili wa kuwatambua unaendelea vizuri mkoani humo.

Mpango huo wa kukata kodi ya majengo mtu anaponunua umeme ulipoanza ulipigiwa kelele na wananchi, lakini kwa sasa umeonekana kuzoeleka.

Akizungumzia mtindo ulioibuka kwa watu kukodi sehemu za maduka na kuweka bidhaa zao na kuziuza kinyemela bila ya kutoa risti, Mtandika alisema mnunuaji atakayekamatwa atapigwa faini ya Sh. milioni 1.5 na anayeuza atalipa Sh. milioni 4.5 na kwamba mwananchi atakayetoa taarifa kuhusu uhalifu huo naye atalipwa.

Alisema lengo la adhabu hiyo ni kuhakikisha kila mnunuaji anaponunua bidhaa anadai risiti na yule aliyeuza anatoa.

Kuhusu wafanyabiashara ndogo ndogo kuondolewa maeneo yasiyokuwa rasmi na kupangwa vizuri hususani mjini, alisema mpango umewasaidia kuwaona na kuwafikia kirahisi wafanyabiashara wakubwa wenye leseni.

"Kwa sasa tunawafikia wafanyabiashara wakubwa walio na leseni na kuhakikisha wanalipa kodi stahiki tofauti na ilivyokuwa hapo awali walipokuwa wamechanganywa na machinga," alisema.

Akizungumzia kodi ya mazao yakiwamo ya samaki ilipitishwa na Bunge hivi karibuni, Mtandika alisema kwa mwezi wanakusanya Sh. milioni 700 kwa mwezi.

Aliongeza kuwa sheria hiyo inamtaka anayenunua mazao yoyote yakiwamo ya chakula na samaki anatakiwa kumkata muuzaji asilimia mbili ya mauzo ghafi na kuiwasilisha TRA.

"Hiyo inatusaidia kuongeza mapato yetu na tukiona hivyo tunamfuata muuzaji na kumwambia kwamba kama ameweza kukatwa asilimia mbili, sasa ajisajili TRA ili awe mlipakodi rasmi na wengi wanakubali na kuanza kulipa.

Kuhusu makusanyo ya kodi kwa mwaka mkoani Mwanza, Mtandika wanatarajia kukusanya wastani wa Sh. bilioni 200.

Alisema kuanzia mwezi Julai hadi Oktoba, mwaka huu, wamefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 50 sawa na asilimia 98 ya lengo walilojiwekea la Sh. bilioni 51 kwa miezi mitatu.

# Daraja la JPM lawapa funzo wahandisi

**Na Jaliwason Jasson,**
MWANZA

WAHANDISI 28 wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET) Tawi la Manyara wamesema uwapo wa maji siyo kikwazo tena cha kuzuia makandarasi kushindwa kujenga miradi mikubwa ya barabara na madaraja ili kusaidia kuimarisha miundombinu.

Walisema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea Daraja la JPM (Kigongo-Busisi) lenye urefu wa kilometa 3.2 na barabara unganishi ya kilometa 1.66, ambalo linajengwa katika wilaya za Misungwi na Sengerema. Mwenyekiti wa IET Tawi la Manyara na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoani Manyara, Mhandisi Bashiri Rwesingisa, alisema lengo la ziara hiyo lilikuwa kuadhimisha mwaka mmoja wa IET toka ianzishwe Oktoba mwaka jana na wameona wafike katika daraja hilo ili wajifunze na kuboresha uwezo wao.

Mhandisi Rwesingisa alisema baada ya kuona daraja hilo linavyojengwa, sasa uwapo wa maji si kikwazo tena kwa makandarasi wanaofanya nao kazi.

"Makandarasi hatutawaruhusu kusimamisha kazi au kushindwa kufanya kazi kwa kisingizio cha kuwapo maji maeneo ya mradi maana tumejifunza namna ya kufanya kazi kwenye maji," alisema.

Pia alisema teknolojia waliyoiona daraja la JPM inatoa funzo kuwa wahandisi wakiungana wakaitumia wanaweza kujenga daraja la kuiunganisha Zanzibar na Tanzania Bara na kuwaondolea usumbufu wananchi ambao ikifika saa 12 jioni wanashindwa kusafiri na boti.

Mwenyekiti huyo aliwataka wahandisi vijana kuwa na uthubutu na ubunifu kwa kupambana na vikwazo ili wawe chachu ya kuleta maendeleo. Alisema huo ni mwanzo wa wahandisi kufanya ziara za kujifunza ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

Naye Katibu wa IET Manyara, Mhandisi Christopher Sahuli, alisema fani ya uhandisi si historia inakuwa kila siku ndiyo maana wameamua kwenda daraja la JPM kujifunza.

"Baada ya kuona madaraja yanavyojengwa kwenye maji, ninao uwezo wa kusimamia mradi vizuri unaojengwa kwenye maji," alisema Mhandisi Sahuli na kuwataka wahandisi vijana kukua kwenye kazi kukubali kuendelea kujifunza na kupenda fani yao.

Mhandisi Dominick Kamugisha kutoka Kampuni ya Wegil Investment alisema sasa anaweza kujenga mradi kwenye maji kwa kuwa mashine inazamishwa chini ya maji inavunja mwamba na kutenganisha tope na maji na hatimaye kuchota maji kwa kuyamwaga na kumwaga zege kwenye mapipa makubwa.

Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja la JPM, Benjamin Michael, akizungumza na wahandisi hao, alisema uwezo wa kujenga daraja hilo umetokana na uzoefu alioupata wa kujenga miradi mikubwa aliyoshiriki ukiwamo mradi wa reli ya kisasa SGR.

Mhandisi Michael alisema mradi huo utakamilika kwa ubora kulingana na mkataba huku akisema daraja litadumu kwa miaka zaidi ya 120.




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, akizungumza wakati akitambulisha kampeni mpya iitwayo Wagiftishe, Gift juu ya Gift, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya wateja wapya na wa zamani wa mtandao wa Tigo. Kushoto ni Mhamasishaji wa kampeni hiyo, Mzee Shayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tigo yakumbuka wateja katika kufunga mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kidigitali hapa nchini, Tigo, imezindua kampeni mpya ya kufunga mwaka inayofahamika kama "WAGIFTISHE GIFT JUU YA GIFT".

Lengo na dhumuni ni kufanya sikukuu za mwisho wa mwaka kuwa za kipekee wa wateja wa Tigo nchi nzima ambapo mteja atapata nafasi ya kushinda simu janja hadi 12 kila siku ndani ya wiki sita.

Kampeni hii ni kwa ajili ya wateja wapya na wazamani wa mtandao wa Tigo ambapo mteja atakayenunua simu janja ya ITEL T20 kwa gharama ya Sh. 89,000 kutoka katika maduka ya Tigo nchi nzima watapata intaneti ya BURE GB 72 kwa mwaka mzima na wakati huo huo ataingia kwenye droo ya kushinda simu janja 12 kila siku na pikipiki moja kila wiki kwa kipindi cha wiki sita.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni hiyo, Meneja Mawasiliano kutoka Tigo, Woinde Shisael alisema kuwa:

"Kampeni hii inalenga kuongeza watumiaji wa simu janja nchini ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kutoka asilimia 45 mwaka 2021 hadi asilimia 80 kufikia mwaka 2025 . Lakini kama mtandao unaoongoza kwa ubunifu na utoaji wa huduma za kidigitali nchini kampeni hii itawawezesha wateja wetu kujipatia simu janja mpya na za kisasa alikadharika kuwanunulia ndugu, jamaa na marafiki huku wakijipatia mtandao wenye kasi zaidi wa 4G."

"Kwa kipindi chote cha sikukuu za mwisho wa mwaka wateja wa Tigo wamekuwa wakifurahia ofa kabambe za punguzo la bei za simu pamoja na GIFT kemkemu kwa ajili yao na ndugu zao, ambazo tunaamini zinaunganisha familia, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na kudumisha upendo ndio maana tumekuwa tukiendelea kutoa ofa hizi kila mwisho wa mwaka ikiwa kama ishara ya kuwajali na kuwathamini wateja wetu," alisisitiza Woinde.

# Tutuba ataka maadili kwa wakaguzi wa ndani

**Na Benny Mwaipaja,**
ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, amewataka wakaguzi wakuu wa ndani kuzingatia maadili ya kazi zao kwa kujiepusha na vitendo vya rushwa wanapotimiza majukumu yao ili kaguzi wanazofanya ziwe na tija kwa taifa.

Tutuba alitoa rai hiyo jijini Arusha wakati akifunga Mkutano wa Mwaka wa Wakaguzi Wakuu wa Ndani uliowashirikisha wakaguzi 500 kutoka taasisi za umma nchini uliolenga kuweka mikakati ya namna ya kuboresha tasnia ya ukaguzi nchini. Alisema kuwa vitendo vya ukiukwaji wa maadili vinasababisha thamani ya fedha inayotolewa na serikali kwa ajili ya kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi isionekane.

Aidha, amewaagiza wakaguzi hao wakuu wa ndani kwenda kukagua fedha za kampeni ya maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhini ya Uviko-19 na kutoa taarifa serikalini kila mwezi. Katika hatua nyingine, Tutuba ameiagiza Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango kutengeneza moduli ya mfumo wa utekelezaji wa miradi kitaifa itakayotumika kusajili miradi yote inayotekelezwa hapa nchini ili kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo. Alisema hatua hiyo itawasaidia hata wakaguzi wa ndani kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa moduli hiyo itakuwa ikitumika kukusanya taarifa za utekelezaji wa miradi pamoja na picha zinazoonyesha maendeleo ya ujenzi wake hatua kwa hatua.

Kwa upande wake Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG), Athumani Mbuttuka, alisema kuwa mkutano huo umekuwa na manufaa makubwa kwa kuwa umetumika kukumbushana wajibu wa utekelezaji wa mjukumu ya Wakaguzi Wakuu wa Ndani.

Alibainisha kuwa mkutano huo pia umeibua changamoto mbalimbali zinazoikabili tasnia ya ukaguzi ikiwamo uhaba wa watumishi na vitendea kazi mambo ambayo serikali imeahidi kuyafanyia kazi.

Akizungumza kwa niaba ya Wakaguzi Wakuu wa Ndani, Neema Kiure, aliipongeza serikali kwa kuandaa mkutano huo uliotoa fursa kwa wakaguzi hao kujitafakari namna wanavyotekeleza majukumu yao na kuahidi kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya watendaji hao.

Alibainisha kuwa wakaguzi wakuu wa ndani ni jicho la serikali katika kuhakikisha kuwa rasilimali fedha na miundombinu mingine inatumika kama ilivyokusudiwa ili kuleta thamani halisi ya uwekezaji huo wa serikali katika jitihada zake za kuwaletea wananchi maendeleo.



Ukurasa 12

Waziri Gwajima afunguka Ustawi wa Jamii ulivyo mtaji mipango maendeleo




Ukurasa 13

Viongozi wa maeneo mmezidi kubwetekea matatizo yenu

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 19, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

MIAKA 28 YA CWT

**Katibu Mkuu: Tunatangaza ushindi bila silaha kuu ya kugomea serikali**

# Paul Anyakun: Kijana aliyeanzisha utalii simu kuzuru kijiji utamaduni

**Na Mwandishi Wetu**

## • Ni Karamoja Uganda, baada ya janga la Corona

NI kijiji cha aina yake cha utamaduni. Hapo kuna dansi za kitamaduni, pia mifugo na wafugaji vijana. Hiyo ndio taswira inayokukaribisha katika eneo la Karamoja, Kenya.

Kwa muda mrefu hiki kimekuwa kivutio kikubwa cha watalii kutoka maeneo mbalimbali kote duniani, wakiwania kuwasili mahali hapo.

Lakini janga la Corona liliporindima, ndege zikaegeshwa na safari za kimataifa zikakoma kuelekea mahali hapo. Ni eneo sawia na mengine ya kitaliii, kwa maana imeathirika pakubwa na simulizi hiyo ya Corona. Hapo mambo yakawa tofauti, wenyeji ambao walitegemea utalii, nao wakaangukia lindi la umaskini.

Hapo ndipo kijana Paul Anyakun, akabuni wazo mbadala Chini ya mwavuli wa kampuni yake, Destination Nomad Afrika, au DNA kama anavyojulikana na wengi. Alianzisha utalii wa mtandao, kwa kutumia video za simu.

"Awali tulikuwa tunajiuliza mtu ataona vipi video kwa simu na awe anafurahia utalii? Lakini, sasa hauhitaji kulipia ndege au gari na bado unaweza kutalii eneo la Karamoja," anasimulia DNA.



Kijana Paul Anyakun, akiionyesha jambo katika ujuzi wake wa utalii picha. **PICHA: MTANDAO**

Sasa utalii huu unafanywaje? Paul Anyakun anatumia simu kuendeleza utamaduni na kimsingi ni kwamba kama mtu yuko mathalan Marekani au Ulaya, anatembezwa katika kijiji cha kitamaduni cha jamii ya Karamoja kwa kutumia simu yake pekee.

"Wanapolipia ziara ya kitalii na sisi, kwanza kabisa tunauliza ungependa nini? Kwa mfano kama unataka kupanda mlima au kutembelea kijiji cha jamii ya Karamoja. Kisha tunaenda kuangalia kama eneo hilo lina mtandao mzuri wa intaneti.

"Halafu siku ya ziara yenyewe, kwanza tunakupatia taswira na picha ya eneo tulipo, mimi sionekani kwenye video, kisha baada ya kukueleza kuhusu hapo, narudi kwenye kamera sasa, maana watu wanaamini zaidi wanapoona sura na hisi za macho yako unavyojieleza," anaeleza DNA.

Sehemu kubwa ya wateja wake ni wanafunzi kutoka Marekani na mataifa ya Ulaya, ambao hawajahi kufika Afrika. Hapo wanapewa uwezekano wa kutembelea kijiji cha kitamaduni cha Karamoja, wakiwa kwao nyumbani na inakuwa jambo la kusherehekewa sana.

Inatajwa kuwa sawia na biashara nyingine yoyote, utalii wa mtandao una changamoto zake, akifafanua: "Kwanza ni simu, maana unaweza ukawa na simu ya Android kwa mfano, labda video yake si nzuri sana, wewe unamuona mteja vizuri.

"Lakini, mtalii anaona ni kama umemwagiwa maji usoni. Pia, mtandao wetu si mzuri sana katika maeneo mengi ya Afrika na hiyo inafanya kazi hii kuwa ngumu kidogo."

Janga la Corona lilikwamisha kabisa shughuli za utalii katika maeneo mbalimbali duniani, lakini huko Karamoja Mashariki mwa Uganda, Paul Anyakun 'almaarufu' DNA, ametumia ubunifu kuhakikisha bado watalii wanazuru eneo hilo, hata wakiwa kwa majumba mwao.

***• Kwa mujibu wa BBC***

UCHUMI

MIAKA 60 YA UHURU

# Waziri Dk. Gwajima afunguka Ustawi wa Jamii ulivyo mtaji wa mipango maendeleo

• Kila zito aliloamua Nyerere, aliwakabidhi shoka

**Na Mwandishi Wetu**

DESEMBA 9, mwaka huu Tanganyika ambayo kwa sasa ni Tanzania, itatimiza miaka 60 tangu ipate uhuru kutoka kwa mtawala Mwingereza.

Kwa kipindi hicho, serikali kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, imekuwa mstari wa mbele kuchochea ustawi na maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk.Dorothy Gwajima, anajivunia kipindi hicho kuwa serikali imejenga uwezo wa jamii, akijinasibu na utekelezaji miradi mikubwa inayotatua kero za kijamii na kiuchumi.

"Wataalamu wa maendeleo ya jamii wamefanya kazi kubwa ya kuamsha ari ya jamii kushiriki katika miradi ya maendeleo na kuiwezesha jamii kutambua mchango wa serikali kwa maendeleo yao," anaeleza.

Anatoa mfano, katika kipindi kato ya mwaka 2015 hadi 2020, wamewezesha jumla ya kaya 617,100 kuboresha vyoo; kaya 305,724 kuboresha pa kunawa mikono; ujenzi wa madarasa shule za msingi 6,521 na sekondari 2,499; hospitali 67 za halmashauri, pia miradi mingine vijijini na mijini.

### KAMPENI ZA MAENDELEO

Waziri anasema, wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika miaka kati ya 1960 hadi 1980, walikuwa chachu ya kutekeleza kampeni za kitaifa zinazohitaji ushiriki wa jamii.

Anataja baadhi yake ni: Uhuru na Kazi; Siasa ni Kilimo; Kisomo Chenye Manufaa; Azimio la Arusha; Mtu ni Afya; Elimu kwa Wote; Chanjo ya Watoto Wenye Umri Chini ya Miaka Mitano; pia Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto.

"Katika miaka 2019-2021, wataalam hawa wanaendelea kuamsha ari ya jamii kuboresha makazi yao kupitia Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora, ambao hadi sasa jumla ya nyumba 4,008 zimejengwa," anasema.

Dk. Gwajima anasema, jamii ya sasa ina mwamko wa kujiletea maendeleo kwa kuanzisha miradi inayolenga kutatua changamoto zinazowakabili, mfano hai ujenzi wa barabara, maboma ya madarasa, zahanati na vituo vya afya.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizindua ripoti ya Mchanganuo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mkutano wao wa mwaka, jijini Dodoma, Septemba 30, mwaka huu. Kushoto ni Waziri, Dk. Dorothy Gwajima. **NA MPIGAPICHA WETU**

> **"Tangu kipindi hicho wanawake wameendelea kuaminiwa ambapo kwa sasa idadi ya Mawaziri wanawake imefika saba.**

### ULINGO WA MAFUNZO

Dk. Gwajima anasema, wakati sasa ni miaka 60 ya Uhuru, serikali imepanua wigo wa mafunzo kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii, ambao katika zama miaka ya 1960 kulikuwapo chuo kimoja tu cha maendeleo ya jamii - Tengeru, ila kwa sasa idadi 63, kati ya hivyo 12 ni vya umma.

"Kati ya vyuo 12 vya serikali, tisa vinasimamiwa na wizara yangu. Mafunzo hayo yanatolewa kuanzia ngazi ya astashahada hadi shahada ya uzamili, ili kuongeza thamani ya mafunzo yanayotolewa na vyuo vilivyo chini ya Wizara.

" Programu za uanagenzi zimeanzishwa ili kuwaandaa wahitimu kujiajiri na kuajiriwa; programu za ubunifu zinazotoa fursa kwa wanafunzi na jamii inayozunguka vyuo kufanya kazi za ubunifu unaosaidia kutatua changamoto mbalimbali na ajira. Hadi sasa vimeanzishwa vituo vya ubunifu wa kidigitali tisa," anaeleza.

### ULINZI WA MTOTO

Waziri anasema, ili kuimarisha upatikanaji haki, maendeleo na ustawi wa mtoto serikali imeongeza wigo wa kutekeleza masuala ya watoto, kwa kuridhia na kutia saini mikataba ya kikanda na kimataifa.

"Katika kipindi cha mwanzo cha Uhuru wa Tanzania Bara, jukwaa pekee la watoto la kujadili masuala yanayowahusu na kufikisha ujumbe ilikuwa ni kupitia shule, ikijumuisha majukwaa kama chipukizi.

Anasema, ni mfumo ulioshirikisha watoto waliopo shule na kuwaacha walio nje ya hapo, hivyo kutokutoa fursa sawa ya kushirikisha watoto wote.

Waziri anaeleza uanzishwaji wa madawati ya ulinzi wa watoto shuleni yanalenga kuwashirikisha watoto katika kutoa taarifa za ukatili dhidi yao, ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wakosaji.

### SERA YA MAENDELEO

Waziri anasema, Sera ya Maendeleo ya Mtoto iliandaliwa mwaka 1996 na kufanyiwa mapitio mwaka 2008, ikiainisha haki tano za msingi kwa mtoto: Kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kutobaguliwa.

Pia, anataja Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inayosimamia kupatikana haki za mtoto, ikijumuisha ulinzi wake, dhidi ya ukatili aina zote, huku wizara ikiratibu huduma za simu bila malipo '116' kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio hayo dhalimu.

Anasema katika kuimarisha huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara inaratibu uandaaji Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22 hadi 2025/26) inayolenga kumlea na kumkuza mtoto kwa utimilifu wake.

"Wizara imeanzisha vituo vya kijamii 30 vya mfano, lengo ni kujenga vituo hivyo katika vijiji na mitaa yote nchini. Vilevile, serikali imesajili jumla ya vituo 2,133 vya kulelea watoto wadogo mchana kwa ajili ya kutoa huduma za malezi na uchangamshi wa awali.

"Aidha, ili kukabiliana na changamoto za afya na maendeleo kwa vijana balehe, wizara iliratibu uandaaji na inasimamia utekelezaji wa ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe (2021/22 hadi 2024/25).

"Lengo likiwa kukabiliana na changamoto zinazowakabili vijana balehe wenye umri wa 10 hadi 19 katika maeneo ya VVU/UKIMWI, mimba za utotoni, ukatili, lishe bora, kuendelea kuwa shuleni na kujengewa ujuzi ili kupata fursa za kiuchumi," anasema.

Lingine linaloendana na huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na msaada wa kisaikolojia, zimekuwa zikitolewa kwa njia ya mtandao kuwafikia wananchi wanaokabiliwa na shida hiyo.

### ULINZI WA WATOTO

Eneo lingine lililoimarisha huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto katika mazingira hatarishi, kwa kuhakikisha kuwapo programu za malezi mbadala kama vile ya watoto wa kambo.

Pia, anataja kuasili watoto, malezi ya watu wa kuaminika kwa watoto walio nje ya malezi ya familia na wanaokabiliwa na vitendo vya ukatili katika familia.

"Kwa sasa serikali inaratibu na kusimamia jumla ya makao ya watoto 239 ikilinganishwa na moja lililokuwapo mwaka 1960 na serikali kwa kushirikiana na shirika la Abbot Fund imejenga Makao ya Taifa ya Watoto katika eneo la Kikombo," anasema.

Katika miaka 60 ya Uhuru, serikali imeweka utaratibu wa maofisa ustawi wa jamii, kusimamia upatikanaji haki kwa watoto katika mahakama 147 za watoto, ambazo zilianzishwa nchini kupitia Sheria ya Mtoto 2009.

### MAENDELEO KINAMAMA

Waziri Dk. Gwajima anasema, serikali imefanya jitihada za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ndani na nje ya nchi, yeye akiwa mnufaika.

"Baraza la kwanza la Mawaziri mara baada ya uhuru hakukuwa na mwanamke. Mwanamke wa kwanza kuwa Waziri ilikuwa mwaka 1965, ambayo Lucy Selina Lameck Somi aliteuliwa kuwa waziri mdogo wa Shirika na Maendeleo ya Jamii.

"Tangu kipindi hicho wanawake wameendelea kuaminiwa ambapo kwa sasa idadi ya Mawaziri wanawake imefika saba,"anasema waziri, akitaja idadi ya wabunge wanawake imeongezeka kutoka sita mwaka1961 hadi kufikia 145 wa mwaka jana.

Kwa mujibu wa Dk. Gwajima, serikali katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru imewawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchumi, ikiwamo kuwezesha nyenzo mbalimbali kama kutolewa mikopo isiyo na riba, inayotokana na kutengwa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri).

### KUTOKOMEZA UKATILI

Anasema serikali imeimarisha mifumo ya kupambana na kuzuia vitendo vya ukatili wa wanawake na Watoto kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto MTAKUWWA (2017/18 2021/22).

"Jitihada hizi zimewezesha kamati 18,186 mpaka sasa kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa, Madawati ya Jinsia na Watoto 420 katika vituo vya Polisi, Madawati ya Jinsia 153 katika Jeshi la Magereza na Dawati katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya kupambana na vitendo vya rushwa ya ngono kupitia Kampeni ya "Vunja Ukimya."


### USIMAMIZI NGO'S

Dk.Gwajima anataja eneo la mashirika yasiyo ya kiserikali haikutambulika katika kipindi cha Uhuru kwa kuwa taasisi zilizojulikana kipindi hicho, ni za dini na vyama vya wafanyakazi.

Anasema, badaaye ndani ya miaka hiyo 60 ya Uhuru, hatua zilichukuliwa kuzijumuisha asasi hizo zisizo za kiserikali kusajiliwa na kutambulika rasmi, kupitia Sheria Namba 24 ya Mwaka 2002, akiwasilisha takwimu idadi yake kuongezeka kutoka asasi 404 za mwaka 2005 hadi 11,731 mwezi uliopita, ikiichangia kuleta maendeleo kwa jamii.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Viongozi wa maeneo mmezidi kubwetekea matatizo yenu






**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

MIONGONI mwa semi maarufu za Waswahili ni huu usemao 'mgeni njoo mwenyeji apone'. Maana yake ni kwamba, mgeni yeyote afikapo nyumbani kwa mtu huja na riziki.

Siku mgeni afikapo kwa mtu huja na neema. Ndipo siku atachinjwa mnyama au ndege kwa furaha. Ndiyo siku familia itabadilisha mlo, kwani kuna mgeni hivyo aibu hufichwa.

Siku ya mgeni hata, vyombo ambavyo havikuwa vinatumika hutolewa kabatini na kuoshwa kwa ajili ya mgeni. Mgeni ana heshima ya pekee, mgeni huheshimisha familia na kujaza furaha, ingawa husababisha gharama.

Mgeni afikapo, ndipo pia hutokea fursa ya kujuzana mambo mengi ya atokako. Lakini usishangaea kagundua vitu ambavyo wewe unavyo kwako na hujui kuwa vinaweza kukusaidia kimaisha. Mgeni ana jicho la kuona. Je, ni kweli? Yawezekana.

Historia inatuambia kuwa enzi hizo, zama zile, walikuja wageni nchini na kugundua vitu tulivyokuwa tukiishi navyo, bila kujua umuhimu au thamani yao. Walipobaini hivyo vitu wakaviita kwa majina yao.

Walipofika Uchagani, wakakuta mlima ambao wenyeji waliuita Kilemakyaro, lakini wao kwa kushindwa kutamka, wakauita Kilimanjaro na kujitangaza kuwa wameugundua wao, kana kwamba Wachaga walikuwa mawe yasiyogundua nini ni kile na manufaa yake. Kina Speke hao wakafanya yao.

Wageni wengine wakasafiri mpaka Kanda ya Ziwa, wakajidai wamegundua ziwa, wakati wenyeji wakiliita Nyanja au Nyanza, wao wakajitapa kuligundua na kuliita kwa jina la malkia wao, Victoria. Nasi tukalikamata hivyo na kuendelea kuliita hivyo hadi leo.

Katika kujitia upofu hata baadhi ya barabara na mitaa tukaiita kwa majina ya Wazungu hao hao, kana kwamba walikuja nayo kutoka kwao. Tukachekelea kumridhisha mzungu, mtawala wetu kwa kubeza majina yetu na kujiita yao.

Wakatumia dini kutuaminisha kuwa majina yetu hayajakaa kistaarabu, hivyo tubadili rasmi majina na kuwa ya kizungu. Tukawana kina Joseph, tukawa na kina Beatrice, wakaja kina Anicetus, kina Martin na wengineo ili mradi mgeni njoo mwenyeji apone. Tukadhani kuitana majina ya kizungu basi ndio tumepona, lakini kumbe kujidanganya tu.

Kwanini dhana hii ikatuganda mpaka leo kwamba bila ya kuja mtu atuonyeshe kitu, hatuwezi kugundua kuwa kipo au kina matatizo haya au yale? Ni nini, ni ugonjwa au kuzubaa tu?

Hivi sababu ni nini hata viongozi wetu wa maeneo wanasubiri wafike viongozi wa kitaifa, ndipo wajue kuwa katika maeneo yao kuna matatizo? Haiingii akilini, kwamba nyumba unayoikalia hujui matatizo yaliyomo mpaka aje mgeni.

Kwanini sasa tukaja na semi kuwa kitanda usichokilalia hujui kunguni wake? Lakini, kwani ni siri ya mtungi siku hizi kata haiijui? Kwanini fimbo ya mbali siku hizi inaua nyoka? Eti pilipili iliyo shamba sasa inatuwasha. Eh, maajabu!

Nilibaki kinywa wazi hivi karibuni, kutokana na ukame uliosababishwa na jua kali linaloendelea kuitesa dunia na hasa nchi yetu, Waziri Mkuu Majaliwa akaamua kwenda Ruvu Chini na Juu kuangalia kulikoni.

Kufika huko, eti ndipo viongozi wa maji na wakazi wa maeneo hayo wakabaini kuwa kuna umwagiliaji unaopunguza maji Mto Ruvu, eti ndipo watu wakajua kuwa ng'ombe wa huko nao wanakunywa maji mpaka basi!

Wao walikuwa wamekaa kimya, wanasubiri mgawo wa maji uanze, huku wakishinikiza Watanzania wanaotumia maji ya Mto Ruvu wafunge siku tatu wakiomba mvua inyeshe, utadhani ingesaidia!

Hivi nyie viongozi tuliokuchagueni na ninyi mlioteuliwa, nini mnafanya kwenye maeneo yenu katika kumsaidia Chifu Hangaya kukabiliana na matatizo ya wananchi wake? Mnasubiri Mwenge eti uone matatizo, mnasubiri ziara za wakubwa kubaini matatizo yenu kweli? Aibu kuu. Alamsiki!

UCHUMI

MIAKA 28 YA CWT

# Katibu Mkuu: Tunatangaza ushindi bila silaha kuu ya kugomea serikali

- Hisa za walimu benki yao; mkopo bila riba
- Vyeo vinapanda 'kilaini', pesa za likizo...

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAREHE mosi ya mwezi huu Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kimetimiza miaka 28 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993.

Msingi wa kuwapo kwake ni kutekeleza madhumuni ya kujenga nguvu ya pamoja katika kudai haki, maslahi na mazingira bora ya kazi, ikiwalinda wafanyakazi, dhidi ya uonevu na ukandamizaji wa mwajiri kazini, pia inasuluhisha migogoro inayohusu ajira zao.

Lingine ni kuwawezesha wafanyakazi kutoa maoni yanayohusu magumu yao kazini na kuongeza tija ya kukabiliana na vikwazo vya uzalishaji, kujadili na kupendekeza miundo bora ya utumishi.

Hadi sasa, zaidi ya nusu ya wanachama wa CWT ni walimu wa umma nchini. Kihistoria, miaka ya nyuma ilizoeleka kuwa kada inayoelemewa na kero kama za fedha za likizo, malimbikizo ya mishahara na kutopandishwa madaraja kwa wakati.

Hata hivyo, serikali imeamua kuingilia kati na kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na kero na hapo uongozi wa CWT unaweka wazi siri ya kada hiyo kuwa na utulivu.



Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, akizungumza katika maadhimisho ya miaka 28 ya CWT. Nyuma yake ni Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

**KATIBU CWT AFUNGUKA**

Katibu Mkuu wa CWT Taifa, Deus Seif, anasema utulivu uliopo sasa kwa walimu ni sehemu ya mafanikio ya chama kutumia meza ya mazungumzo kuwasilisha hoja serikalini bila ya mgomo.

"Chama cha wafanyakazi kimeanzishwa kwa lengo la kumtetea mfanyakazi, kuna staili mbalimbali za kila uongozi unaoingia. Mimi na viongozi wenzangu tulikuja na mtindo tofauti kidogo, tukitaka stahiki zetu, hatuendi kwenye magazeti tukaandika, hatunyanyui bango kwamba walimu hawajalipwa likizo.

"Sisi tunakaa meza moja na mwajiri na kuna mengi yamefanyika. Kwa mfano, kulikuwapo ukomo kwenye upandishaji vyeo, chama kiliondoa.

"Huu mfumo wa TAMISEMI wa kukusanya madai ni mafanikio yetu tulitaka uwepo mfumo huu ambao utaondoa udanganyifu," anasema, akitaka mafanikio ya kuwa na wanachama zaidi ya 260,000.

"Benki ya Walimu ni mafanikio ya CWT na kutengeneza faida kuwatetea walimu katika masuala ya kisheria, licha ya kwamba hatuhamasishi wao kutenda makosa, lakini yanatokea. Hakuna namna kama suala la utoro. Zaidi ya kesi asilimia 95 tumeshinda," anasema.

> **Sisi tunakaa meza moja na mwajiri na kuna mengi yamefanyika. Kwa mfano, kulikuwapo ukomo kwenye upandishaji vyeo, chama kiliondoa.**

Katibu huyo anasema chama cha wafanyakazi silaha yake ya mwisho ni mgomo. Anafafanuzi: "Haya yote tunayofanikiwa yanaanzia meza ya mzungumzo. Ukiangalia historia yetu ya chama, tumewahi kugoma, lakini hatujawahi kupata tija kwenye migomo hiyo.

"Kulikuwa na shida, watumishi wengine walikuwa wanapanda vyeo bila kusoma, lakini walimu pekee walikuwa na ukomo. Huko kote tumewahi kugoma, mbona ukomo haujawahi kuondolewa? Ukomo umeondolewa kwa kutumia meza ya mazungumzo," anasema.

Anaongeza "Sisi tunaamini tumechagua njia sahihi na tunashirikiana na serikali. Juzi wamepandishwa watumishi wa umma vyeo zaidi ya 230,000, kati ya hao 210,000 ni walimu.

"Sasa kwanini tuseme hatuna mafanikio, kama kwa miaka miwili wamepandishwa walimu kiasi hicho na kupandishwa cheo ni zaidi ya nyongeza ya mshahara?

"Sasa niwaambie walimu wagome kwa sababu gani? Vyeo wamepanda, madai ya mishahara wanalipwa, madai ambayo si ya mshahara ndio takwimu zimekusanywa kwa ajili ya kulipwa anajigamba na kuendelea:

"Sasa niwaambie walimu waende barabarani kufanya nini? Kipi ambacho tumeshindwana mezani? Ukweli ni huu "tumewin' (tumeishinda) serikali kwa kutumia 'roundtable' (mazungumzo mezani)."

Anasema CWT hivi inawapeleka masomoni walimu kujiendeleza na wana imani Rais Samia Suluhu Hassan, ataendelea kutatua kero katika kada hiyo kutokana na maono yake katika elimu, ikiwa ni kipaumbele cha uongozi wake.

**RAIS CWT**

Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani, anasema licha ya mafanikio, bado kuna kero ya kutofanikishwa fedha za likizo na uhamisho kwa baadhi ya walimu, hali kadhalika kutolipwa bima ya maisha kwa waliojiunga na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

"Kuna walimu wengi wameingia kwenye mikataba na bima zimeiva, lakini hawalipwi kwa jinsi walivyoingia nao mikataba. Hatuelewi limeanza kutengeneza hasara au imekuwaje?" Anasema huku akiwasilisha rai kwa serikali kuingilia kati kisheria, akiendelea:

"Sisi tunaangalia mkataba, labda unasema umeingia kwa miaka 10 na baada ya hapo utapata fedha zako na faida, lakini muda unafika unazungushwa."

Kuhusu uhamisho, Rais huyo analalamika kwamba kinachojiri kinawakwaza walimu, wanapohama kituo kimoja cha kazi kwenda kingine. Anaahidi CWT kuendelea kufuatilia utatuzi wake.

**MAFUNZO KAZINI**

Naibu Katibu Mkuu CWT, Maganga Japhet, anasema katika miaka hiyo 28, wamewaendeleza walimu kitaaluma wakiwa kazini, kupitia miradi mbalimbali ya mafunzo inayoendeshwa na chama.

Anataja mojawapo, ni unaotekelezwa kwa kushirikiana na Denmark, pia shirika kutoka Uingereza, inayowaandaa walimu kufundisha madarasa ya awali ili kukidhi sera ya elimu iliyopo; mtoto sharti kupitia darasa la awali, kabla hajajiunga na elimu ya darasa la kwanza.

Japhet anasema, ni mradi unaotarajiwa kusukuma maendeleo ya elimu ya awali, kukiwapo wastani walimu 500 kutoka wilaya za Chemba na Mpwapwa, mkoani Dodoma, waliokwishapatiwa mafunzo ya stashahada ya kufundisha elimu ya awali.

Anaeleza ni mradi usiothiri vipindi vya mwalimu darasani, kwa sababu yanatolewa kipindi cha likizo, huku akitamka: "Ukimwandaa mtoto darasa la awali, akiingia darasa la kwanza anakuwa tayari kupokea maarifa."

Anasema CWT inatekeleza mradi wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara kukiwapo walimu 700 wameshanufaika nao, lengo ni kumuimarisha mwalimu katika eneo hilo.

**UWEKEZAJI ULIVYO**

Mweka Hazina wa CWT Taifa, Abubakar Alawi, anajisifu chama chake kimefanikiwa kuwa na majengo ya ofisi kila mkoa.

"Kuna majengo yanatengeneza mapato kama jengo la Mwalimu House na sehemu ya fedha zinazopatikana zimetumika kwa matumizi mbalimbali," anaeleza.

Anaainisha kuwapo Sh. bilioni moja zimetumika kununua hisa kwenye Benki ya Walimu na Sh. milioni 920 zilipelekwa kwenye SACCOS walimu wanakopo bila ya riba. Kila mkoa imepelekwa Sh. milioni 40.

Kiasi kingine Sh. bilioni 11 kimetumika kununua hisa za wanachama wote kwenye benki hiyo. Hao ni waliokuwa kwenye mfumo wa malipo mishahara hadi mwaka 2015.

na familia zao.





# Kampuni mpya 174 zatoa ajira 57,650

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema kampuni 174 zimesajiliwa katika maeneo ya EPZ na SEZ na kuwekeza mtaji wa Dola za Kimarekani bilioni 2.23.

Amesema kupitia uwekezaji huo jumla ya ajira 57,563 zimezalishwa, hivyo kuwanufaisha Watanzania wengi.

Prof. Mkumbo alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta za viwanda na biashara katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo ya EPZ/SEZ ili kuhakikisha mazao ya kilimo, misitu, mifugo, uvuvi na madini yanayozalishwa nchini yanaongezwa thamani na kutengeneza ajira kwa Watanzania badala ya kusafirishwa kama malighafi kwenda nje.

"Kwa sasa serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji ambaye ni kampuni ya CMPort kutoka China na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman ili ujenzi wa eneo maalum la kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo SEZ) uanze mapema iwezekanavyo," alisema.

Pia alisema mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la taifa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo wakati wa uhuru mwaka 1961 sekta ya viwanda ilikuwa ikichangia asilimia 3.5 ya pato la taifa.

"Hadi kufikia mwaka 2015 mchango wa sekta hiyo ulikuwa asilimia 7.9 kutokana na jitihada ya serikali za kuhamasisha ujenzi wa viwanda mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la taifa uliongezeka na kufikia asilimia 8.5 ya pato la taifa. Mwaka 2019 na mwaka 2020 mchango wa sekta ulishuka kidogo hadi asilimia 8.4"alisema

Kuhusu mchango wa sekta ya viwanda kwenye ajira alisema imeendelea kuongezeka ambapo mwaka 1961, ilichangia asilimi tisa ya ajira zote nchini.

"Hadi kufikia mwaka 2015, ajira katika sekta ya viwanda zilikuwa zimeongezeka na kufikia 254,786. Aidha kutokana na msukumo mkubwa wa ujenzi wa uchumi wa viwanda, idadi ya ajira imeongezeka zaidi na kufikia ajira 482,601 mwaka 2021," alisema Prof. Mkumbo

Pia alisema wizara hiyo imeandaa mwongozo wa uwekezaji katika mitaa ya viwanda nchini ili kurahisisha taratibu za uwekezaji katika mitaa ya viwanda na kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

# Waitara ataka ufuatiliaji nyumba za TBA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, ameitaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuboresha kitengo cha ufuatiliaji ili kujua nyumba ambazo zimekuwa zikipangishwa kwa watumishi wa umma na wao kuwapangisha watu wengine.

Waitara alisema hayo juzi katika ziara yake ya kukagua nyumba 20 katika eneo la Kisasa na nyumba 150 zilizoko Nzuguni jijini Dodoma ambazo zinajengwa na TBA kwa ajili ya watumishi wa umma.

"Ule mpango mtu anapewa nyumba anakaa kisha onaondoka anapewa mtu mwingine bila makubaliano kama mkataba aliingia na watu wa TBA akitaka kuondoka ni lazima ukague nyumba wakati anaingia ilikuwaje na wakati anatoka imekuwaje.

"Nyumba zetu hizi ni nzuri lazima kuwe na kitengo cha kufuatilia kuona matengenezo yakoje, hili mtoe uzito. Lazima mboreshe kitengo cha ufuatiliaji. Mfano Dodoma mahitaji ni makubwa lakini wanataka pia nyumba iboreshwe," alisema

Waitara aliipongeza TBA kwa kujenga nyumba bora na zenye kiwango kinachokubalika. Alisema ujenzi wa nyumba hizo unatarajiwa kukamilika Septemba, mwakani.

"Tunatarajia Rais atakuwa anafuatilia. Bahati nzuri mnajenga nyumba na mitambo ya kokoto na matofali ipo hapa hapa, hivyo hakutakuwa na kisingizio. Nimefurahi mnafanya kazi na mradi utaisha mwakani mwezi wa tisa na viongozi watarajia kuzitumia nyumba hizi," alisema.

Kuhusu kodi, Naibu Waziri alisema nyumba hizo ni za watumishi na zimejengwa na serikali, hivyo gharama zake zitakuwa ndogo.

"Nyumba hizi ni za watumishi na zimejengwa na serikali ili kumpunguzia ukali wa maisha mtumishi tukipangisha watumishi wakatosha tutapangisha watu wengine," alisema.

Waitara pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi mkoani Dodoma.

"Kwanza nimshukuru sana Rais Samia kwa kutoa fedha. Ametoa fedha nyingi kwa mfano pale nyumba 20 makisio ni Sh. bilioni tano na ameishatoa fedha yote kwa hiyo watu wa TBA kazi kwao tunatarajia nyumba zikamilike kwa wakati.

"Eneo hili mnaloliona ni ekari 680 ni eneo kubwa tunakusudia kujenga nyumba za kawaida zaidi ya 3,000 katika eneo hili na zitakuwa nyumba za ghorofa. Kwa hiyo huu ni mradi mkubwa ambao tumeanza kama sehemu ya mfano tunatarajia watu wa TBA wakifanya vizuri zaidi Mheshimiwa Rais ataendelea kutoa hela," alisema.

Meneja wa Wakala wa Majengo Mkoa wa Dodoma, Victor Balthazar, alimshukuru Naibu Waziri kwa kutembelea mradi huo huku akiahidi watatekeleza kwa wakati.

Pia aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huo na kusema kwa mkoa wa Dodoma mahitaji ya nyumba kwa watumishi wa umma ni makubwa.



Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio na mwelekeo wa sekta ya sheria, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katambi:Serikali imeazimia kuendeleza wanawake

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amesema serikali imeazimia kuendelea kufungua fursa kwa wanawake nchini katika kufanya biashara.

Mbali na fursa hizo amesema inatarajia pia kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya kukuza mitaji, kufungua masoko na kuwasaidia vitendea kazi.

Katambi alibainisha hayo jana alipokuwa akizindua mradi wa Waendeleze unaoratibiwa na serikali kwa kushirikiana na Ubalozi wa Uholanzi nchini.

Alisema serikali imeendelea kutoa fursa kwa wanawake kujiendeleza kibiashara ili kuinua uwezo wao na kuwawezesha katika kuchangia maendeleo ya taifa.

Pia alisema mradi huo wa Waendeleze ni moja ya jitihada za serikali pamoja na ushirikiano mzuri na wadau wa maendeleo ambao unalenga kuwainua wanawake ili kufanya biashara na kufikia malengo.

Katika kufanikisha mradi huo, alisema Ubalozi wa Uholanzi nchini umewezesha mafunzo kwa wafanyabiashara wanawake kwa kushirikiana na taasisi ya uongozi kutoka Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Mashariki.

"Tumeshuhudia hapa wafanyabiashara wanawake wanaojishughulisha na mambo mbalimbali ya uzalishaji mali yakiwamo kilimo, ufugaji, usindikaji na kadhalika namna mafunzo hayo yalivyowasaidia kufungua fursa nyingi ikiwa ni pamoja na kukuza mtandao wa biashara zao na masoko," alisema

Katambi aliwasihi wanawake walionufaika na mafunzo hayo kutoa elimu na kuwa mfano wa kuigwa katika maeneo wanayofanya biashara ili kuwapa hamasa wengine kujiunga.

Aliwahimiza kutumia fursa hiyo kuwahamasisha wenzao ikiwa ni pamoja na vijana na watu wenye ulemavu kuchangamikia fursa ya mikopo ya asilimia 10 kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ili kuanzisha na kuendeleza shughuli au miradi itakayowaingizia kipato na kutimiza ndoto zao.

Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer, alisema serikali ya Uholanzi itaendelea kushirikiana katika kuboresha na kuendeleza wafanyabiasha wanawake nchini kupitia mradi huo wa Waendeleze.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Lindam, Zuhura Muro, alisema mradi huo umewawezesha wafanyabiashara wanawake kupata hamasa ya kuchangia pato la taifa na pia kupitia shughuli zao za kiuchumi wameweza kutoa fursa za ajira kwa wengine.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Kilimo Biashara kutoka Benki ya NMB, Issack Masusu, alisema benki hiyo imepunguza riba katika eneo la sekta ya kilimo na kilimo biashara kutoka asilimia 18 hadi 10.





# Wakulima wa mboga wataka kiwanda

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa mboga katika Bonde la Ilolo Jijini Mbeya, wameiomba Serikali kujenga kiwanda cha kuchakata zao hilo ili kuwapo soko la uhakika na kujikwamua na umasikini

Wakizungumza na Nipashe jana, walisema kuwa wamekuwa wakizalisha aina mbalimbali ya mboga na kuuza kwa bei chee kutokana na kukosekana kwa masoko ya uhakika.

Jane Mwakifwamba alisema endapo Serikali itajenga kiwanda cha kuchakata mboga kutawezesha kuzalisha kwa tija ikiwa ni pamoja na kipata masoko ya nje ya nchi na kutumia fursa ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

"Tunaomba pia tuwezeshwe kupata mikopo yenye riba nafuu kutokana na kilimo kuhitaji mtaji mkubwa hususan upatikanaji wa pembejeo kama mbolea na dawa ya kuua wadudu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema Serikali imetenga zaidi ya Sh. 1.8 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mboga katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani. Alisema kuwa wakati mchakato huo ukiendelea pia wanaendelea kuboresha miundombinu ya soko la machinga lengo ni kutanua wigo wa shughuli za kiuchumi.

"Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miradi mikubwa ya kimkakati hususan Sekta ya elimu, afya miundombinu jambo ambalo litawezesha taifa kuwa na watu makini,"alisema.

Aliwasisitiza wananchi kuendelea kujiunga kwenye vikundi mbalimbali vya wajasiriamali ili kupata mikopo ambayo itawawezesha kupata mitaji itayosaidia kuendesha biashara zao za kuchakata mazao baada ya kuongeza thamani.

Alisema Serikali kupitia idara ya maendeleo ya jamii inaendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mikopo inayotolewa ikiwa ni pamoja na nidhamu ya matumizi au ununuzi wa vifaa ambavyo vitarahisisha shughuli za uzalishaji mali.

Wakati huo huo, Mkuu wa Mkoa amewataka wananchi kujitokeza katika zoezi la sensa ya watu na makazi ili kuwezesha serikali kufanya vyema katika miradi ya maendeleo.



Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalwega, akizungumza wakati wa kikao kuhusu masuala mbalimbali yanayowakabili watu wenye ulemavu, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Shule 2 za wenye ulemavu kujengwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

Mkoa wa Mbeya unakusudia kujenga shule maalum mbili za msingi na sekondari kwa watu wenye ulemavu, lengo likiwa ni kukabiliana na idadi kubwa ya watoto wanaosoma sambamba na kusoma katika mazingira yenye utulivu.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera wakati wa kikao cha kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili watu wenye ulemavu mkoani humo.

Alisema wanakusudia kujenga shule za kisasa kwa watoto wenye ulemavu ambazo zitakuwa na miundombinu rafiki ya kujisomea ili kuweza kutimiza malengo yao.

Alisema shule hizo zitakuwa za mfano nchini na kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali watakamilisha ujenzi huo.

Alisema wameona vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo watoto wenye ulemavu ikiwamo madarasa na miundombinu mengine ya kujisomea watoto hao sasa ujenzi wa shule mbili msingi na sekondari utakuwa mwarobaini wa kutatua shida hiyo.

Kwa upande wake, Ofisa Taaluma Mkoa wa Mbeya, Wilbroad Yanga, alisema serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema Shule ya Msingi yenye mahitaji maalumu ya Katumba II iliyoko wilayani Rungwe imetengewe shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni, Sh. milioni 90 ujenzi wa jengo la utawala pamoja na vyumba vitatu vya madarasa lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa watoto shuleni hapo.

Alisema Shule ya Msingi Katumba II inakabiliwa na tatizo kubwa la miundombinu ya madarasa kutokana na mrundikano wa wanafunzi ambao wanatoka maeneo mbalimbali nchini.

# Ushirikiano wanahabari na wanasheria watakiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VYOMBO vya habari vimehimizwa kuwa na ushirikiano wa karibu na wanasheria ili kuwezesha kuchukua hatua za kisheria pale inapotokea mwanahabari anafanyika vitendo vya udhalilishaji ikiwemo mitandaoni.

Sambamba na hilo, viongozi kwenye vyombo vya habari wakiwamo wahariri wameshauriwa kuwa mstari wa mbele kuwapa mwongozo wa njia sahihi za kuchukua waandishi pale wanapodhalilishwa kupitia mitandao ya kijamii.

Hayo yalibainishwa na mmoja wa wakufunzi, Chelu Matuzya kwenye semina ya mafunzo ya udhalilishaji wanahabari mitandaoni iliyofanyika jana kwa njia wa mtandao wa Zoom ikiandaliwa na Shirika la Women News.

Chelu aliliwataja waandishi wa habari wanawake kuwa kwenye kundi linaloongoza kwa kudhalilishwa kupitia mitandao ya kijamii hatua aliyosema inahitaji kuwepo kwa mikakati madhubuti ndani ya vyombo vyao ili kuwalinda.

Alisema vyombo vingi havina Miongozo inayomlinda au kumwongoza moja kwa moja mwanahabari anapodhalilishwa na hivyo kumfanya mhusika kushindwa kupata njia ya kutatua matatizo yake anapokutana na udhalilishaji.

Alisema hatua zinazopaswa kuchukuliwa na vyombo vya habari nchini ni kuwa na wanasheria wanaoweza kuwa msaada kwa waandishi wanapodhalilishwa na pia wataalamu wa utoaji ushauri wa kisaikolojia ili kumwezesha mhusika kutoumizwa zaidi na jambo alilofanyiwa.

Mratibu wa Shirika la Women in News Tanzania, Joyce Bazira, alisema waliamua kuandaa semina hiyo kutokana na uchunguzi kuonesha hali ya udhalilishaji wa waandishi wa kike kupitia mitandao ya kijamii ni kubwa na jamii haichukui hatua kudhibiti.

Bazila alisema kutokana na kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji waandishi wanawake wapo baadhi yao wameathiriwa na kufika hatua ya kuacha kujituma katika kazi kutokana na kujiona hawako kwenye mazingira rafiki.

Mkurugenzi wa Shirika la Women in News, Jane Godia alisema udhalilishaji wa mitandaoni mara zote hufanywa na watu wanaokuzunguka ambao miongoni mwao ni watu unaoweza kuwa unafanya kazi nao na unawaamini kama sehemu ya watu muhimu kwako.

Alisema ni muhimu elimu ya kupinga udhalilishaji wa aina hiyo iendelee kutolewa kwa jamii ili kuwafanya waandishi wa habari hususani wanawake kuendelea kutoa mchango wao kwa jamii kupitia kalamu zao.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki wa semina hiyo,Martha Fatael alisema jambo linalosikitisha zaidi ni kuona udhalilishaji mitandano unatokana na mhusika kujituma katika kazi hatua inayosababisha wadau kukupa kazi nyingi lakini wasiopenda mafanikio wanakuhusisha na mahusiano ya aina nyingine ikiwemo ya kingono.

Hata hivyo Martha aliwataka waandishi wa habari wanawake kutokatishwa tamaa na udhalilishaji wa aina yoyote kutokana na kazi zao badala yake wazidi kufanya bidii kazini wakati wadau kwama Women News wakiendeleza juhudi za kuelimisha jamii.





# ZAECA yaziomba asasi kutoa elimu ya rushwa, uhujumu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), ACP Ahmed Makarani, amezitaka asasi za kiraia kuisaidia serikali katika kutoa elimu ya rushwa na uhujumu uchumi kwa maslahi ya taifa.

Alisema endapo wanajamii watapatiwa elimu hiyo, lengo la serikali la kutokomeza uhalifu huo litafanikiwa na kuisaidia Zanzibar katika kutekeleza vyema miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa sekta ya jamii, ulioshirikisha wadau mbalimbali wa asasi za kiraia, uliofanyika Mjini Zanzibar.

Makarani alieleza kuwa asasi za kiraia zipo karibu zaidi na wanajamii, hivyo zina uwezo mkubwa wa kutoa elimu na kuizuwia rushwa pale inapotendeka, jambo ambalo litaisaidia mamlaka hiyo katika kupambana na uhalifu huo.

Aidha, alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoathiriwa na rushwa na uhujumu uchumi, hivyo ni vyema kwa kila mwanajamii kutoa ushirikiano wa dhati kwa mamlaka hiyo ili kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa maslahi ya wananchi.

Akiwasilisha mada kuhusu uzuiaji rushwa na nafasi ya sekta za jamii katika kupambana na rushwa, Ofisa Elimu kutoka ZAECA, Futari Mzee Ali, alisema asasi za kiraia ziwe mstari wa mbele katika kutoa taarifa sahihi za rushwa na uhujumu uchumi ili hatua za kisheria kuchukuliwa haraka na mamlaka husika.

Alisema mikataba mbalimbali ya kimataifa inazitaka asasi za kiraia zishirikishwe katika mapambano dhidi ya rushwa, kutokana na umuhimu mkubwa wa kusaidia katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kuwa karibu zaidi na wanajamii.

Hata hivyo, alisema ipo haja kwa kila asasi ya kiraia kumlinda mtoaji taarifa ili kuhakikisha usalama wake, kwa lengo la kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa.

Wakitoa maoni baadhi ya washiriki katika mkutano huo walisema ipo haja ya utoaji wa elimu ya rushwa kwa kila mwananchi ikiwamo rushwa ya ngono pamoja na kuondoa dhana potofu ya kuwaona hawana maana baadhi ya watumishi wasiochukua rushwa wakati wa kutoa huduma.

# Safari za moja kwa moja Ufaransa-Zanzibar zampa matumaini Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kurejea kwa safari za anga za moja kwa moja kutoka Ufaransa hadi Zanzibar kupitia Shirika la Ndege la Air France kutatoa msukumo mkubwa katika sekta ya utalii na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi Ikulu jijini Zanzibar, alipokutana na Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hijilaoui, aliyefika kujitambulisha na kupata fursa ya kuzungumzia miradi mbalimbali, ambapo nchi hiyo itaisaidia Zanzibar.

Alisema kurejea kwa safari za mashirika kadhaa ya ndege duniani kumeifanya Zanzibar kupokea idadi kubwa ya watalii, hivyo kuisaidia kuimarisha sekta ya utalii ambayo imeathirika kutokana na janga la Uviko-19.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inahitaji kampuni mbalimbali zenye azma ya kuwekeza katika sekta ya nishati ya umeme, ikiwamo wa jua ili kuongeza uwezo wake wa kusambaza nishati hiyo kwa wananchi.

Alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo la upungufu wa huduma za majisafi na salama, hususan katika maeneo ya hoteli za kitalii, hivyo misaada katika sekta ya maji ni jambo la muhimu.

Dk. Mwinyi aliipongeza Ufaransa kwa ushiriki wake wa kusaidia miradi mbalimbali ya kijamii na maendeleo na kubainisha hatua hiyo itafanikisha na kuharakisha azma ya Zanzibar kukuza uchumi wake kupitia uchumi wa bluu.

Alimweleza Balozi huyo maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Mafuta Mangapwani, inayohusisha bandari tofauti na kubainisha fursa kadhaa za uwekezaji zilizopo, hivyo akatoa wito kwa wawekezaji kutoka Ufaransa kuwekeza.

Alisema azma ya Serikali ya kuanzisha kikosi maalum cha ulinzi wa watalii (Tourism Police) ni kuhakikisha watalii wote wanaofika nchini wanakuwa salama muda wote.

Naye Balozi Nabil aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uhusiano na ushirikiano wake na Ufaransa, huku akipongeza uwapo wa amani na utulivu sambamba na kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kutimiza mwaka mmoja wa uongozi wake.

Balozi Nabil aliahidi kuwashajihisha wawekezaji kutoka Ufaransa kuwekeza Zanzibar katika miradi mbalimbali ya maendeleo.




Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Dar es Salaam, ACP Abdi Issango (wa tatu kushoto), akipokea kitabu cha mafunzo ya usalama barabarani kutoka kwa Meneja Mawasiliano Mwandamizi wa TBL, Amanda Walter, wakati wa uzinduzi wa programu ya simu ya usalama wa barabarani iliyobuniwa na kampuni hiyo kwa kushirikiana naTaasisi ya Mafunzo naUtafiti yaUmoja waMataifa (UNITAR), mkoani humo juzi. Wengine ni maofisa kutoka jeshi hilo na TBL. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yapania kuiboresha sekta ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe, amesema, azma ya Serikali ya Zanzibar ni kuyapanga maeneo ya mikoa yote ya Unguja na Pemba ili kuepusha ujenzi holela na kupunguza kasi ya migogoro ya ardhi.

Alisema pia serikali itahakikisha inaweka haiba nzuri ya maeneo ya wananchi na uwekezaji na kupanga matumizi yanayozingatia uwiano wa idadi ya watu mijini na vijijini.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwaka mmoja wa uongozi wa Dk. Mwinyi kupitia wizara hiyo. Alisema katika kuimarisha sekta ya makazi, wizara yake inaendelea na juhudi ya kuziboresha nyumba za maendeleo, kutafuta kampuni na wadau wa makazi ili kuwekeza katika sekta ya nyumba.

Alisema kwa sasa mchakato wa ujenzi wa nyumba za maendeleo unaendelea kwa kushirikiana na sekta binafsi katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Alieleza kuwa katika jitihada za kuimarisha mapato na kuzingatia mchango wa sekta ya ardhi kwa maendeleo na uchumi na jamii, wizara yake imefanya uhakiki wa maeneo ya uwekezaji na kubaini uwapo wa changamoto katika maeneo hayo ikiwamo maeneo mengi kutoendelezwa.

"Wapo ambao hawana mikataba ya ardhi na wengine wanatumia hati za haki ya matumizi ya ardhi (CRO) katika maeneo ya uwekezaji," alisema.

Waziri Pembe alisema kutokana na changamoto hizo, ametoa indhari ili kuhakikisha kwamba ardhi inanufaisha serikali na wananchi wake ambapo miongoni mwa idhari hizo wawekezaji wote wa kigeni ambao hawajaendeleza maeneo yao na wanayo mikataba ya ukodishwaji ardhi, wanatakiwa kuendeleza maeneo yao kwa kipindi cha miezi sita.

Alisema kwa wananchi na wawekezaji wazalendo wanatakiwa kuendeleza maeneo yao kwa kpindi cha mwaka mmoja na baada ya hapo kama hakuna uendelezaji wa maeneo hayo yatafutwa na kurudi serikalini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**kiwanja kina uzwa** mkoni kagela wilaya ya bihalamulo kina ukubwa wa hekali 20 bei yake ni Tsh 10,000,000/= kwa maelezo zaidi pigs namba 0624636584 au 0733089917

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

## TANGAZO

### GODDY & TONNY TRADERS LIMITED

**Registration No. 143987272**

116576502

Bodi ya wakurugugenzi kwa pamoja na wamiliki wakampuni ya **GODDY & TONNY TRADERS LIMITED** wameamua kufunga kampuni yao baada ya kushindwa kuendesha biadhara waliyokuwa wamekusudia kuifanya. Bodi hiyo pia imemchangua bwana **JUMANNE SAMWEL GODWIN** kuwa msimamizi wa zoezi la ufungaji wa kampuni hiyo. Kwa yeyote mwenye madai na kampuni hii awasiliane na bwana **JUMANNE SAMWEL GODWIN.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYA YA KAHAMA**
**SHAURI LA MADAI NO.46 LA 2021**

**IBRAHIM YUSUPH JUMA ULOTU.......................................................MDAI**

**DHIDI YA**

1. **SHILOLE LUSWETULA**
2. **MKWANGU MIHAYO**
3. **MICHAEL TUNGU@WINGU**
4. **JOHN NYERERE**
5. **MAWAZO RASHID@MCHELEMCHELE**
6. **WINLET KAKULIMA**
7. **DAUD FUMBU**
8. **MASELE JOHN**

**KUITWA SHAURINI WADAIWA**

**KWA;**

1. **SHILOLE LUSWETULA**
2. **MKWANGU MIHAYO**
3. **MICHAEL TUNGU@WINGU**
4. **JOHN NYERERE**
5. **MAWAZO RASHID@MCHELEMCHELE**
6. **WINLET KAKULIMA**
7. **DAUD FUMBU**
8. **MASELE JOHN**

**POPOTE MLIPO.**

116576602

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake hapa Mahakama ya Wilaya ya Kahama katika shauri tajwa hapo juu, ambalo litasikilizwa tarehe 22/11/2021.

Unatakiwa kuhudhuria mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 22/11/2021, saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa, siku hiyo ni siku ya kusikilizwa kwa shauri hili ni lazima uje na vielelezo vyote vinavyohusiana na shauri hili kwa ajili ya kujibu madai haya.

Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri laweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu ya upande mmoja bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii tarehe 17 mwezi Novemba, 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA.**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya SINGIDA**
**Kituo cha UTEMINI Mkoa SINGIDA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 136/2021**

**Jina la Mdai ISSA KIMARO**

**Jina la Mdaiwa OMARY MUGHENYI.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa OMARI MUGHENI**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA FEDHA Tsh. 7,000,000.**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 mwezi 11 mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kusikiliza shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu,na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii yatolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 mwezi 11 mwaka 2021.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.180 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANTHONY LONGINI MINDE Of Hamvu within Dodoma City**

**And**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAGDALENA JOSEPH MAUKI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 7/12/2021
Dated at Dodoma this 16 Day of November,2021.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAZARO WILLIAM MAINOYA**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T727BMN ,**
Engine **No. 1G687DG57**
Chassis **No. GX110502311D**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/550255/2021.**
Imeripotiwa na MUNA **ABDALLAH TALIB.**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# IAEA yadai Iran inazalisha urani iliyorutubishwa

**Vienna,** AUSTRIA

SHIRIKA la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA), linasema Iran inaendelea kuzalisha urani iliyorutubishwa mno, kuliko ukomo uliowekwa chini ya makubaliano ya nyuklia ya mwaka 2015.

Ripoti ya hivi karibuni ya IAEA juu ya suala hilo inakadiria kuwa nchi hiyo ilimiliki kilogramu 17.7 za urani iliyorutubishwa hadi usafi wa asilimia 60 kufikia Novemba 6, mwaka huu.

Kiwango hicho ni cha juu zaidi kuliko ukomo wa asilimia 3.67 uliowekwa chini ya makubaliano hayo.

Ripoti hiyo ilisema Iran haikuiruhusu IAEA kuweka kamera mpya za ufuatiliaji kwenye kituo cha nyuklia kilichoko jirani na Tehran kunakotengenezwa baadhi ya mashine za urutubishaji.

Ofisa mwandamizi wa serikali ya Iran, alisema Mkurugenzi Mkuu wa IAEA, Rafael Grossi, ataizuru nchi hiyo kuanzia Jumatatu ijayo.

Anatarajiwa kuzungumza na upande wa Iran juu ya vizuizi vya ukaguzi wa shirika hilo. **NHK**

# ...Wafungwa 3 waliotoroka jela ya Kamiti Kenya wakamatwa

**Nairobi,** KENYA

HATIMAYE wafungwa wanaohusishwa na ugaidi ambao walitoroka Gereza la Kamiti, Jumatatu, wamekamatwa.

Musharaf Abdalla maarufu Alex Shikanda, Joseph Ouma na Mohammed Ali Abikar walikamatwa katika eneo la Kitui.

Kwa sasa washukiwa hao wanasafirishwa kurudi jijini Nairobi.

Walitoroka katika gereza hilo linalolindwa zaidi baada ya kutoboa ukuta wa jela hiyo.

Baadaye walitumia nguo aina ya blanketi na waya kutengeneza kamba ambazo walitumia kupanda kuta mbili ndefu.

Hatua hiyo ilisababisha baadhi ya maofisa wa Gereza la Kamiti kukamatwa kwa madai ya kuwasaidia wahalifu hao kutoroka.

Jumatano, Rais Uhuru Kenyatta alimwagiza Waziri wa masuala ya Ndani, Fred Matiangi, kuhakikisha wanatumia kila mbinu kuwakamata wahalifu hao hatari.

Alivitaka vitengo vyote vya upelelezi kuwawajibisha maofisa wote waliodaiwa kuhusika na kutoroka kwao.

Kulingana na gazeti la Daily Nation, vitengo vya usalama katika kaunti ya Kitui vilikuwa vimewekwa katika hali ya tahadhari baada ya wakazi wa eneo hilo kuwaona wafungwa hao watoro.

Kamanda wa Polisi Kaunti ya Kitui, Leah Kithei, jana alithibitisha kwamba vitengo vyote vya usalama katika eneo hilo, wakiwamo machifu na manaibu wao walikuwa wamewekwa katika hali ya tahadhari.

"Habari hiyo pia imesambazwa kwa wenzetu katika kaunti jirani ya Tanariver na Garissa," Kithei aliiambia Daily Nation.

"Iwapo ni kweli ni wao, bila shaka tutawakamata, ni muda tu kabla ya hilo kufanyika". **BBC**



Mwanamfalme Charles na mkewe Camilla, walipotembelea eneo la kale, Umm Qais, lilioko jirani na Ziwa Tiberias, mjini Jordan, juzi. Familia hiyo ya kifalme ipo nchini Misri baada ya miaka 15 kupita na safari ya kwanza barani Afrika tangu mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19. **PICHA: AP**

# Kamishna wa Magereza Kenya ashtakiwa

**Nairobi**, KENYA

KAMISHNA Mkuu wa Magereza Kenya, Wycliffe Ogalo, amefunguliwa mashtaka baada ya Rais Uhuru Kenyatta, kumfuta kazi.

Hatua hiyo inakuja baada ya magaidi watatu kutoroka gerezani mapema wiki hii.

Kamishna Ogalo alitiwa nguvuni muda mfupi baada ya Rais Kenyatta kutangaza kufutwa kazi kwake.

Ogalo na maofisa wengine wakuu wa gereza lenye ulinzi mkali la Kamiti, walikamatwa na kuhojiwa na maofisa wa kitengo cha upelelezi.

Hayo yanajiri baada ya magaidi watatu kutoroka gereza hilo, Jumanne.

Uamuzi wa kuwakamata maofisa hao wakuu wa magereza, unajiri muda mfupi baada ya Rais Kenyatta kukutana na maofisa wakuu katika Wizara ya Usalama wa Taifa wakiongozwa na Waziri Fred Matiangi.

Kwenye kikao hicho cha faragha, ilifichuliwa kuwa, maofisa wa magereza walikuwa na kasoro katika utendaji kazi wao.

Ogalo amehudumu kwa muda mrefu katika serikali na alikuwa amehudumu kwenye cheo hicho kwa kipindi cha miaka miwili.

Alichukua nafasi ya Isaya Osugo ambaye aliacha sifa ya kutekeleza mabadiliko kadhaa kwenye idara hiyo.

Rais Kenyatta alimteua na kushuhudia kamishna mpya Brigedia mstaafu John Kibaso Warioba akila kiapo cha utendaji kazi katika Ikulu ya Nairobi.

"Niko katika mchakato wa kuchukua nafasi ya mtangulizi wangu, kwa sasa hayo ndio naweza kuwafahamisha."

Hata hivyo kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, Idara ya kuwaajiri maofisa wa polisi, imekanusha habari za kutiwa nguvuni kwa kamishna Ogalo, ikisema ni za kupotosha.

Idara hiyo ilisema hatua iliyochukuliwa ilikuwa ya kupisha uongozi mpya.

Hata hivyo wakili wa Ogalo, Assa Nyakundi alithibitisha kuwa, Ogalo aliachiliwa baadaye bila ya masharti kutoka kwa makao makuu ya Idara ya Upelelezi.

Nyakundi alisema kuwa mteja wake alitakiwa kuondoka bila ya maelezo yoyote.

Kuondoka kwa Ogalo, ni nafuu kwa baadhi ya maofisa wa kitengo hicho cha kurekebisha tabia, hasa katibu mkuu Zeynab Mohammed ambaye hawakuelewana.

"Brigedia mstaafu Warioba, ni mtumishi wa umma mwenye uzoefu wa siku nyingi na tunaamini anaweza kuifanya kazi hii."

Maofisa tisa wa magereza wapo rumande baada ya kutoroka kwa magaidi hao waliokuwa wanatumika vifungo vya ugaidi.

Rais Uhuru pia aliamwagiza Matiang'i kutumia kila njia kuwakamata magaidi hao waliotoroka kwenye Gereza la Kamiti.

Maofisa waliohusika kuwatorosha magaidi hao pia wameonywa kuwa watawajibika, pindi watakapopatikana.

Aidha, maofisa waliokuwa kazini, wakati wa tukio hilo wametakiwa kusimamishwa kazi ama kuhamishwa.

Magaidi hao walitoroka baada ya kuchimba shimo na kuruka uzio wa gereza hilo lenye ulinzi mkali kwa kutumia kamba. **DW**

HABARI MICHEZO

# COCA-COLA KWANZA YAANDAA TAMASHA LA 'BIRIANI NA COKE'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya vivywaji baridi ya Coca-Cola Kwanza inatarajia kuzindua kampeni ya 'Biriani Friday na Coka' ambapo wapishi wa biriani zaidi ya 15 kutoka Dar es Salaam watashiriki katika tamasha litakalofanyika kesho kwenye viwanja vya Posta hapa jijini.

**Wapishi hao wataonyesha ufundi wao wa mapishi ya biriani lengo likiwa kuwapa nafasi wateja wao kupata ladha tofauti tofauti huku wakisindikiza vyakula hivyo na vinywaji vya Coca-Cola.**

Akizungumzia kuhusu kampeni hiyo na tamasha, Meneja Biashara na Masoko wa Coca-Cola Kwanza, Wahida Mbaraka alisema kampeni ya Biriani Friday na Coke imekuwapo kwa takribani miezi sita sasa ikiwa na malengo ya kuendeleza utamaduni wa misosi na Coca-Cola.

Wahida alisema kampuni yao imekuwa ikitembelea wateja wao ambapo ni wapishi na waandaji wa biriani kwa kila Ijumaa na kupata wasaa wa kuwapatia wateja wao wa 'biriani Coke ya baridi pale wapatapo chakula kwenye migahawa yao ili kuonja muunganiko mzuri uliopo kati ya biriani na pale unaposhushia na Coca-Cola.

Aliongeza kwa kusema kampeni yao hiyo imefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya, na imekuwa na mwitikio mkubwa ambao umepelekea kuandaa tamasha la kukutanisha wadau wote wa biriani na Coke.

Aliongeza tamasha hilo ambalo litafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi, litakuwa ni la bure na wakazi wote wa Dar es Salaam na mikoa jirani wanakaribishwa kushiriki ili kujionea ubunifu huo wa mapishi.

"Kwa wale watakaoingia usiku ambapo mwisho utakuwa ni saa 6:00 usiku, watapaswa kuingia kwa kiingilio cha Sh. 3000 za Kitanzania, lakini watapata kinywaji cha Monster Energy ambacho pia kinasambazwa na Kampuni ya Coca-Cola kwanza," Wahida alisema.

Katika kupamba tamasha hilo la Biriani na Coca-Cola, burudani za muziki kutoka kwa wasanii mbalimbali wa hapa nchini wakiwamo Isha Mashauzi, Weusi, Baba Levo, Baddest, Dulla Makabila, Stamina, bendi ya Twanga Pepeta na Dj D Ommy atakayesimama katika kuendesha burudani hiyo watatumbuiza.

Tamasha la biriani na Coke limeandaliwa na Kampuni ya Coca-Cola Kwanza kwa lengo la kuwapa wateja wao nafasi ya kuonja muunganiko ulipo kati ya Coke na Biriani na kampuni hiyo imewahakikishia wakazi na washiriki wote wa tamasha kutakuwa na ulinzi wa kutosha, sehemu nzuri za kupaki usafiri wao pamoja na huduma za dharura katika viwanja vya posta.

# Mlandege, Malindi vitani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MIAMBA ya soka visiwani hapa, Mlandege wanatarajia kukutana na Malindi katika mechi ya Ligi Kuu PBZ Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan kuanzia saa 1:00 usiku.

Timu hizo kongwe ndio hufuatiliwa zaidi na mashabiki wa mchezo huo visiwani hapa.

Kuelekea mchezo huo, kila upande umesema wanatarajia mchezo huo utakuwa mgumu lakini wamejiandaa kupata alama tatu.

Kocha Msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah Salum, alisema timu yake ni kubwa na wamejiandaa kufanya vyema katika mchezo huo ingawa lolote linaweza kutokea.

Salum alisema amejipanga kufanya vizuri ili kuwapa raha mashabiki wao ambao wamehamasika kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo.

Naye Kocha Msaidizi wa Malindi, Abdul Salehe Abdallah, alisema ni ngumu kutabiri matokeo ya mchezo huo ambao anaamini utakuwa na upinzani mkubwa.

"Siwezi kusema kama nitapoteza au nitashinda kutokana na upinzani mkubwa uliopo katika ligi hii msimu huu, lakini sisi tumejiandaa vizuri kuendeleza rekodi yetu," alisema Abdallah.



Wasanii wa bendi ya Mjomba wakionyesha umahiri wao wa kucheza sarakasi katika maonyesho ya Wiki ya Huduma ya Fedha yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BMT yaishtukia TPBRC, Mghana

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo Taifa (BMT), limeitaka Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), kufanyia kazi katiba yao bila kusahau kuweka kipengele kinachohusisha utoaji wa leseni kwa mabondia ambao si Watanzania.

Hoja hiyo ilitolewa baada ya kuwapo kwa bondia raia wa Ghana, Richard Lartey ambaye anasimamiwa na Mtanzania, Jay Msangi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano cha BMT, Najaha Bakari, alisema baraza hilo lilikutana na viongozi mbalimbali wa ngumi na kuelekeza kuwasilisha maelezo kuhusiana na shughuli wanazozifanya.

Najaha alisema pia serikali ilisikiliza mapendekezo yaliyotolewa na viongozi hao kuhusiana na utoaji wa leseni kwa mabondia wa kigeni ambao wanapewa mapambano na waandaaji wa hapa nchini.

"Tumewasikiliza na kuwataka kuyaandika mapendekezo yao kwa maandishi na kukabidhi BMT, tumewataka kuweka kipengele hicho katika katiba yao, kipengele ambacho hakipo katika katiba ya sasa ya TPBRC," alisema Najaha.

Aliongeza baada ya kupata utetezi kuhusu sakata la Lartey kushiriki pambano la kimataifa kwa kutumia leseni ya Tanzania, ndipo serikali itatoa uamuzi wake na kumaliza sintofahamu ambayo imeendelea kutawala kwa wadau wa mchezo huo.

Lartey ambaye ni bingwa wa zamani wa Shirikisho la Ngumi la Kimataifa la WBO katika uzito wa juu, anadaiwa aliwahonga viongozi wa TPBRC ili kupata leseni iliyomwezesha kucheza pambano lililofanyika Novemba 3, mwaka huu, nchini Urusi dhidi ya bondia, Abdulkarim Emily.

Lartey alipoteza pambano hilo kwa KO katika raundi ya kwanza, lakini tetesi zikidai mabosi wa TPBRC walipokea rushwa ya Dola za Marekani 30,000 ili apoteze pambano hilo lililopeleka mamlaka ya ngumi Urusi kumfungia kucheza mchezo huo nchini humo.

Mapema Aprili, mwaka huu, Mamlaka ya Ngumi Ghana (GBA), ilimfungia Lartey kujihusisha na ngumi nchini humo baada ya kughushi barua yenye nembo ya mamlaka hiyo ikimruhusu kwenda kucheza pambano la kimataifa Ujerumani na hivyo alilazimika kupata kibali cha nje ya taifa lake ili kuendelea kupigana.

## ZISIKUPITE

### HAALAND AZIGONGANISHA

KLABU za Manchester United na Chelsea zimepata nguvu zaidi za kumshawishi mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 21, ambaye mkataba wake utamruhusu kuondoka kwa ada ya pauni milioni 64 msimu ujao, huku Real Madrid ikikiri nyota huyo raia wa Norway ataelekea Ligi Kuu England. ***(Sun)***

### MADRID YAONYESHA NGUVU

REAL Madrid inapanga kutunishiana misuli na klabu za Chelsea, Manchester City na Paris St-Germain kwa kumwongeza, Erling Haaland, na mshambuliaji Mfaransa wa PSG Kylian Mbappe, 22, kwenye safu ya ushambuliaji ambayo tayari ina Mbrazil Vinicius Junior, 21. ***(AS)***

### NEWCASTLE YAJIPANGA

NEWCASTLE United inapanga kumsajili mlinzi Mholanzi Stefan de Vrij, 29, na kiungo wa Croatia, Marcelo Brozovic, 28, kutoka Inter Milan mwezi Januari, pamoja na kipa wa Lazio Mualbania Thomas Strakosha, 26. ***(Times)***

### POGBA NJIA MOJA

WAKALA wa Paul Pogba, 28, amegusia kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa anaweza kuondoka Manchester United ifikapo Januari, kabla mkataba wake kumalizika majira ya kiangazi. ***(Rai, via Goal)***

### OLMO AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Manchester United inajiandaa kupambana na Barcelona kwa ajili ya kuwania huduma ya winga wa Timu ya Taifa ya Hispania anayecheza RB Leipzig, Dani Olmo, 23. ***(El Nacional)***

### CHELSEA YAMKERA RUDIGER

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, amekua akikasirishwa na ofa ya mkataba wa hivi karibuni pale Chelsea, ambao haukidhi matakwa yake, kuna upungufu ama tofauti ya kiasi cha pauni 60,000 cha mshahara anaotaka kulipwa kwa wiki. ***(Bild, via Sun)***

### LACAZETTE KITAELEWEKA

ARSENAL wako tayari kumpa mkataba mfupi mshambuliaji wake Mfaransa Alexandre Lacazette, 30, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu. ***(Athletic, via Sun)***


### DANJUMA AZUIWA

KLABU ya Villarreal ina mpango kugomea ofa zote zinazotaka kumsajili winga wa Uholanzi, Arnaut Danjuma, 24, ifikapo Januari huku Liverpool ikimfuatilia mshambuliaji huyo wa zamani Bournemouth. ***(Football Insider)***

### SOLSKJAER KUTIMULIWA

KLABU ya Manchester United imeanza mpango wake wa kuleta mbadala wa Ole Gunnar Solskjaer, huku chaguo lao kubwa ni kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers. ***(Manchester Evening News)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA NJIA NYEUPE KUSAJILIWA MADRID

## ●●● Real Madrid ndiyo inatajwa iko kwenye nafasi nzuri ya kumnasa...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imekata tamaa juu ya uwezekano wa kumbakiza kiungo wake, Paul Pogba na Real Madrid wana "nafasi kubwa" kumnasa raia huyo wa Ufaransa, kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la Marca la jana Alhamisi limeandika.

Majaliwa ya Pogba yameendelea kuzusha mjadala hapo kwenye dimba la Old Trafford na kuna uwezekano mkubwa kiungo huyo wa zamani wa Juventus akaondoka mwishoni mwa msimu huu.

Huku mkataba wake ukiwa unafikia tamati mwishoni mwa msimu, Manchester United sasa wanaonekana kukata tamaa ya kumbakisha kikosini mwake huyo.

**United mpaka sasa iko katika sintofahamu iwapo Mfaransa huyo atabakia klabuni hapo ama ataondoka na kwenda kutafuta maisha kwenye timu nyingine.**

Manchester United wanaamini kwamba, Pogba ana uwezekano mkubwa wa kujiunga na Real Madrid, klabu ambayo imekuwa ikimwania kiungo huyo kwa muda mrefu.

Pogba mkataba wake wa sasa unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu na hakujawa na majadiliano ya hivi karibuni kuhusu kusaini mkataba mpya hapo Old Trafford.

Licha ya Pogba kuwaniwa na Real Madrid, lakini amekuwa akihusishwa na klabu yake ya zamani ya Juventus, pamoja na Paris Saint-Germain na Barcelona.


MECHI KALI
HOME
AWAY
MONACO
2.21 | 3.33 | 3.43
LILLE

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS.686

# MAN CITY YAFIKIRIA KUMSAJILI DE JONG



**MANCHESTER,** England

TIMU ya Manchester City imeripotiwa inakaribia kukamilisha usajili wa kiungo wa Barcelona, Frenkie De Jong ifikapo Januari, 2022.

Kwa mujibu wa kituo cha televisheni cha El Chiringuito cha Hispania, kiasi cha pauni milioni 75 zitatosha kukamilisha dili hilo.

De Jong mwenye umri wa miaka 24 alihamia Barcelona akitokea Ajax kwa ada ya pauni milioni 65.

Kuna uvumi kwamba dili la kubadilishana na Raheem Sterling linaweza kufanyika, lakini klabu hiyo ya Hispania inahitaji kuchangisha fedha.

Hata hivyo, Manchester City waliripotiwa mwanzoni mwa wiki hii kwamba, hawana mpango wowote wa kumwachia Sterling kuondoka klabuni hapo.

Sterling, nyota wa Timu ya Taifa ya England, amekuwa hana nafasi kwenye kikosi cha kwanza msimu huu chini ya kocha, Pep Guardiola na hivyo kuibua uvumi anaweza kuondoka katika dirisha la Januari au mwishoni mwa msimu huu.

# Laporta: Messi, Iniesta wanaweza kurudi

**BARCELONA,** Hispania



RAIS wa Barcelona, Joan Laporta hajaondoa uwezekano wa Lionel Messi na Andres Iniesta kurudi klabuni hapo kwa siku zijazo.

Akizungumza katika tukio la utambulisho wa mlinzi mkongwe, Dani Alves mbele ya mashabiki 10,000 pale Camp Nou juzi, Laporta alibainisha kurudi kwa beki huyo wa kulia wa kimataifa wa Brazil kunaweza kufanya nyota wengine wengi kurudi hapo miaka ijayo.

Iniesta aliondoka Barca na kusajiliwa katika klabu ya nchini Japan ya Vissel Kobe mwaka, 2018 huku deni la karibia euro bilioni 1.2 lilimaanisha kwamba, Blaugrana hao wasingeweza kumpa mkataba mpya Messi, na hivyo kumfanya raia huyo wa Argentina kuhamia Paris Saint-Germain, Agosti.

"Siwezi kuondoa uwezekano huo," alisema Laporta wakati alipoulizwa kuhusu uwezekano wa Messi na Iniesta kurudi klabuni hapo.

"Imetokea kwa Dani, na nataka kumshukuru yeye kwa sababu ameona hali ya klabu ilivyo na ametaka kuja kusaidia."

Alves ndio usajili mpya chini ya kocha mpya, Xavi, na amesaini mkataba utakaomweka hapo hadi mwishoni mwa msimu huu, lakini hataruhusiwa kucheza hadi Januari.

"Pia napenda kumshukuru kwa kukubali kuchukua mshahara mdogo kutokana na hali yetu ya kiuchumi.

"Tunakwenda kumaliza hili tatizo, na yeye amefanya jitihada kubwa. Natakiwa kutambua mchango wake," aliongeza Laporta.

"Watu hawa wameifanya klabu hii kuwa kubwa. Messi na Iniesta ndio kabisa, siwezi kutabiri kuhusu majaliwa yajayo, kwa kuwa bado wanacheza, lakini wameifanya klabu kuwa kubwa.

6,934,380

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20.11.21 | 18:00 | Burnley vs Crystal Palace | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 2. 20.11.21 | 18:00 | Aston Villa vs Brighton | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 3. 20.11.21 | 18:00 | Newcastle vs Brentford | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 4.20.11.21 | 18:00 | Wolverhampton vs West Ham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 5. 20.11.21 | 18:00 | Hull City vs Birmingham | 2.63 | 3.12 | 2.63 |
| 6. 20.11.21 | 18:00 | Reading vs Nottingham | 2.89 | 3.18 | 2.39 |
| 7. 20.11.21 | 20:00 | Lazio vs Juventus | 2.78 | 3.36 | 2.48 |
| 8. 20.11.21 | 20:45 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 9. 20.11.21 | 22:45 | Fiorentina vs AC Milan | 3.09 | 3.39 | 2.26 |
| 10. 21.11.21 | 15:00 | Brest vs Lens | 3.03 | 3.43 | 2.26 |
| 11. 21.11.21 | 17:00 | Salernitana vs Sampdoria | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 12. 21.11.21 | 17:00 | Troyes vs St Etienne | 2.35 | 3.34 | 2.94 |
| 13. 21.11.21 | 17:00 | Metz vs Bordeaux | 2.42 | 3.28 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 19 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2249 | Kenya Commercial Bank vs Tusker | 1.95 | 3.13 | 3.76 |
| 14:00 | 5378 | Benfica U23 vs CF Belenenses U23 | 1.63 | 3.85 | 4.43 |
| 16:00 | 1152 | Tanzania Prisons vs Mbeya Kwanza FC | 2.32 | 2.50 | 3.71 |
| 16:00 | 1762 | Al Masry Club vs Pyramids | 3.75 | 3.40 | 1.94 |
| 16:00 | 3020 | Ruvu Shooting vs Simba | 9.00 | 4.40 | 1.39 |
| 16:00 | 3050 | Peterborough United Reserve vs Barnsley U23 | 1.95 | 3.81 | 3.09 |
| 16:00 | 3738 | Leeds United U23 vs Chelsea U23 | 2.03 | 3.81 | 2.89 |
| 16:00 | 4237 | Polisi Tanzania vs Coastal Union | 2.33 | 2.85 | 3.14 |
| 16:00 | 5375 | Talaea El Gaish vs Ghazl EL Mahallah | 2.08 | 3.25 | 3.50 |
| 17:00 | 3726 | Atalanta Youth vs Cagliari Youth | 1.78 | 3.86 | 3.57 |
| 17:00 | 4378 | AC Milan Youth vs Juventus Youth | 3.13 | 3.27 | 2.11 |
| 18:30 | 5160 | Ismaily SC vs Zamalek | 5.73 | 3.85 | 1.56 |
| 18:30 | 5590 | Enppi Club vs Smouha Club | 3.46 | 3.01 | 2.20 |
| 19:00 | 5610 | Zenit St Petersburg vs Nizhny Novgorod | 1.10 | 8.22 | 21.54 |
| 20:30 | 1296 | Hannover vs Paderborn | 2.74 | 3.38 | 2.38 |
| 20:30 | 4440 | Chernomorets Odessa vs Dynamo Kiev | 21.15 | 8.07 | 1.08 |
| 21:00 | 5588 | Al Ahly Cairo vs Arab Contractors | 1.14 | 7.27 | 16.70 |
| 22:00 | 2176 | Birmingham U23 vs Wolverhampton U23 | 3.27 | 3.84 | 1.87 |
| 22:00 | 3056 | Telstar vs ADO Den Haag | 3.11 | 3.65 | 2.04 |
| 22:00 | 3252 | Roda Kerkrade vs Jong AZ Alkmaar | 1.37 | 4.89 | 6.65 |
| 22:00 | 3309 | Fulham U23 vs Stoke City U23 | 1.69 | 4.10 | 4.40 |
| 22:00 | 3588 | NAC Breda vs Jong Utrecht | 1.46 | 4.60 | 5.48 |
| 22:00 | 3654 | Jong Ajax vs FC Volendam | 2.55 | 3.72 | 2.36 |
| 22:00 | 4220 | Helmond Sport vs SBV Excelsior | 4.19 | 3.90 | 1.70 |
| 22:00 | 4583 | Den Bosch vs FC Oss | 2.17 | 3.52 | 2.94 |
| 22:00 | 4913 | Dordrecht vs De Graafschap | 8.39 | 5.85 | 1.26 |
| 22:00 | 4928 | Almere City vs Maastricht | 1.45 | 4.68 | 5.46 |
| 22:00 | 5155 | Emmen vs Jong PSV | 1.36 | 4.87 | 6.82 |
| 22:00 | 5699 | Derby County U23 vs Manchester United U23 | 3.08 | 3.95 | 1.92 |
| 22:30 | 1168 | KAA Gent W vs Standard Liege W | 2.50 | 3.75 | 2.50 |
| 22:30 | 1271 | FC Schaffhausen vs FC Aarau | 2.38 | 3.47 | 2.55 |
| 22:30 | 2144 | Augsburg vs Bayern Munchen | 12.94 | 7.76 | 1.16 |
| 22:45 | 1297 | Bray Wanderers vs UCD Dublin | 3.00 | 3.24 | 2.19 |
| 22:45 | 1319 | Sligo Rovers vs Bohemians FC | 3.23 | 3.23 | 2.08 |
| 22:45 | 2027 | The New Saints vs Newtown AFC | 1.35 | 4.81 | 6.73 |
| 22:45 | 2313 | Finn Harps vs Longford Town | 1.36 | 4.53 | 6.94 |
| 22:45 | 2471 | QPR vs Luton Town | 2.23 | 3.29 | 3.05 |
| 22:45 | 3496 | Cardiff Met Uni. vs Aberystwyth Town | 1.70 | 3.62 | 4.25 |
| 22:45 | 3724 | Lynx FC vs Manchester 62 FC | 1.03 | 20.00 | 27.00 |
| 22:45 | 3731 | Dundalk FC vs Derry City | 1.84 | 3.43 | 3.76 |
| 22:45 | 3804 | Waterford Utd vs St Patricks | 2.94 | 3.37 | 2.16 |
| 22:45 | 4133 | Mechelen vs Brugge | 3.90 | 3.70 | 1.82 |
| 22:45 | 4514 | Bala Town vs Flint Town United | 2.06 | 3.51 | 3.03 |
| 22:45 | 5150 | Shamrock Rovers vs Drogheda Utd | 1.31 | 4.73 | 7.91 |
| 22:45 | 5568 | Queen of South vs Inverness | 3.32 | 3.32 | 2.07 |
| 22:45 | 5666 | Coleraine FC vs Larne | 2.56 | 3.42 | 2.40 |
| 23:00 | 2096 | Fuenlabrada vs Mirandes | 2.21 | 3.13 | 3.23 |
| 23:00 | 4015 | Monaco vs Lille | 2.12 | 3.33 | 3.43 |
| 23:00 | 5557 | Levante vs Athletic Bilbao | 3.36 | 3.26 | 2.20 |
| 23:45 | 5814 | Benfica vs Pacos Ferreira | 1.26 | 5.02 | 9.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# DE LIGT KUONGEZWA MKATABA JUVENTUS




**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeingia kwenye mazungumzo na beki wao wa kati, Matthijs de Ligt kwa ajili ya kumwongeza mkataba mpya ambao utawekwa kwa miamba hiyo ya Turin hadi mwaka 2025.

De Ligt aliwafanya Juventus walipe kiasi cha euro milioni saba kama ada ya uhamisho mwaka 2019 wakati wanamsajili kutoka Ajax, akiwa beki bora kinda duniani kipindi hicho, lakini hajacheza michezo mingi kama alivyotarajiwa.

Msimu huu amejikuta akiwa anawekwa nje mara kwa mara na wakongwe Leonardo Bonucci na Giorgio Chiellini.

Oktoba, mwaka huu alikiri kuwa hana furaha na nafasi anayopata klabuni hapo, huku akihusishwa na kuhamia katika klabu za Barcelona na Chelsea.

Ingawa kuna uvumi huo, lakini Juventus hawana mpango wa kumwachia huku wakizipuuzia taarifa za wakala wake, Mino Raiola.

Mkataba wa sasa De Ligt na Juventus unamalizika mwaka 2022, huku kukiwa na kipengele cha euro milioni 150 kama ada ya kuvunja mkataba.




# *Tottenham hawana mpango na Bale*

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imeripotiwa haina mpango tena wa kumrejesha nyota wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale.

Bale alifanya vyema sana alipokuwa na Spurs miaka ya 2007 hadi 2013, akifanikiwa kufunga mabao 42 kati ya mechi 146 za Ligi Kuu England alizocheza.

Kiwango chake wakati huo kiliwaleta Real Madrid mezani na kufanya biashara ya kumwondoa katika Ligi Kuu England na kumsajili kwa dau nono la euro milioni 91.

Kwa kiasi nyota huyo amepata mafanikio huko Hispania akiwa na Real Madrid, lakini hadi kufikia 2019 akaanza kupoteza radha na kutawaliwa na majeraha, klabu ikataka kumuuza.

Spurs waliamua kumchukua tena kwa mkopo kwa msimu wa 2020/21, lakini hawakukamilisha dili la kumnunua moja kwa moja.

Hata hivyo, licha ya Spurs kuendelea kuhusishwa na saini ya nyota huyu kama mchezaji huru mwaka 2022, pale atakapomaliza mkataba wake na Real Madrid, taarifa kutoka Football London zinaripoti kuwa Tottenham hawana mpango wa kumrejesha tena.

Michezo

Ijumaa Novemba 19, 2021

Nipashe



Pogba njia nyeupe Real Madrid UKURASA 21

# Simba SC, Ruvu tambo zatawala

## Pablo afunguka kikosi chake kiko tayari kusaka pointi tatu huku...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

TUKO tayari, ni maneno mafupi kutoka kwa Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco ambaye kikosi chake kinatarajia kushuka ugenini kuwavaa Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

**Ni mechi ya raundi ya sita ambapo Simba inarejea ikiwa na kumbukumbu ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lililofungwa dakika za majeruhi na Meddie Kagere wakati Ruvu Shooting ilipata kipigo cha magoli 3-1 kutoka kwa vinara wa ligi hiyo, Yanga.**

Mechi ya leo itarudisha kumbukumbu ya mechi ya msimu uliopita kwenye uwanja huo huo, iliyochezwa Juni 3, mwaka huu, Simba ikishinda mabao 3-0, mawili ya John Bocco ambaye anaweza kucheza kwenye mechi ya leo na Chris Mugalu, yeye kwa sasa bado ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili, Pablo, alisema anaitengeneza timu hiyo siyo kwa ajili ya mechi za ndani tu za Ligi Kuu, bali kazi yake ni kuhakikisha anakijenga kikosi imara kitakacholeta ushindani pia katika mechi za kimataifa.

Pablo alisema anahitaji kupata pointi tatu katika mchezo huo kwa ajili ya kuongeza hali ya kujiamini kwa wachezaji wake ambao wameona.

Kocha huyo alisema ingawa hana muda mrefu ndani ya kikosi, anawaamini wachezaji wake wataingia uwanjani kupambana na hatimaye kuhakikisha wanaibuka na ushindi ili kuendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Kurejea kwa baadhi ya nyota waliokuwa katika timu za taifa, kumekiongezea nguvu kikosini chetu kuelekea mchezo huo, tunahitaji kupata pointi tatu katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting, tunajua utakuwa mchezo mgumu na wenye upinzani mkubwa, lakini ushindi ndio kitu tunachohitaji ili kurudisha hali ya kujiamini," alisema Pablo.

Mhispania huyo alisema anafahamu atakutana na timu yenye kucheza soka la ushindani na ameimarisha maeneo tofauti ndani ya kikosi chake ili kutimiza malengo ya timu.

"Nitapata muda zaidi wa kuwaangalia wachezaji wote kwa pamoja, wengine walikuwa katika timu zao za taifa na sasa baadhi wamerejea, nitakuwa na kikosi kamili ambacho ni imara siku si nyingi," Pablo alisema.

Aliongeza jambo muhimu ni kuhakikisha Simba inarejesha heshima yake kwa kuwa imara kwenye mashindano, ikiwamo kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Kombe la FA na kusonga mbele kwenye michuano ya Kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire alisema kikosi chao kipo vizuri na wako tayari kupambana na Simba ili kuzichukua pointi tatu na vile vile kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

"Itakuwa mechi nzuri maana tumejiandaa vizuri na tuko tayari kwa mapambano, nina imani hatutakuwa na kocha mkuu (Boniface Mkwasa), katika benchi lakini amefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo," alisema Bwire.

Aliongeza Ruvu Shooting inawaahidi mashabiki wa soka wa Mwanza na mikoa jirani itaonyesha soka la burudani lakini lenye ubora ambao utawafanya wapate ushindi katika mechi hiyo.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Tanzania Prisons dhidi ya Mbeya Kwanza wakati Polisi Tanzania itawakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itaendelea tena kesho kwa Namungo kuwakaribisha vinara, Yanga wakati Kagera Sugar itavaana na Geita Gold.




Kiungo wa kimataifa wa Simba, Thadeo Lwanga akiwa ameshika tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Uganda. Tuzo hiyo imetolewa na mtandao unaochapisha habari za soka tu nchini humo uitwao Football256.com. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yatamba 'dozi' pale pale

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema 'hesabu' kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo wa kesho wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC zimekamilika na sasa kinachosubiriwa ni muda.

Namungo inatarajiwa kuwakaribisha vinara hao wa ligi kesho kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi, lakini wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa na Simba katika mchezo wao wa mwisho uliochezwa Novemba 3, mwaka huu.

Nabi alisema wachezaji wake wote walioko Lindi wako fiti na anatarajia watafanya kile ambacho amekieleza kwenye programu zake mbalimbali. Kocha huyo alisema kila mchezaji amempa majukumu yake na amewataka wawe na 'heshima' kwa wapinzani wao kwa sababu wanacheza ugenini.

"Tumeshakamilisha programu za mazoezi kwa ajili ya mechi yetu ya Jumamosi, kilichobakia ni maelekezo madogo madogo, katika mpira huwezi kumaliza mechi mpaka utakaposikia filimbi ya mwisho, kwa sasa tunaiangalia kwa awamu ya mwisho kabla ya kuingia uwanjani," alisema Nabi.

Hemed Morocco, Kocha Mkuu wa Namungo, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wamejipanga kuendelea kucheza soka la ushindani na la malengo ili kusaka matokeo mazuri.

Morocco alisema timu zote mbili zinafahamiana, hivyo wanatarajia kuona mechi hiyo itakuwa na ushindani dakika zote 90.

"Ninahitaji kuona wachezaji wangu wanacheza kwa utulivu, wanakuwa makini, endapo watafanya hivyo, pia wakitumia vyema nafasi tutakazotengeneza, Inshaallah tutapata matokeo," Morocco alimaliza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >